MTIHANI WA SHULE ZA KITAIFA NA MTIHANI WA PAMOJA

TATHMINI YA PAMOJA YA MARANDA NA KISII

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

MTIHANI WA KIBAADA MWIGO

102/1 KISWAHILI (INSHA) Karatasi ya 1

INSHA - Kidato cha nne

Januari — Muda: Saa 1 3/4

Jina_____ Nambari ya usajili Mkondo……

Shule Sahihi

Maagizo

1) *Andikajina na nambari yako ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
2) *Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapojuu.*
3) *Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.*
4) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
5) *Kila insha isipungue maneno 400.*
6) *Kila insha ina alama 20.*
7) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili,*
8) *Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa.*

Insha ya lazima

1) Umesoma tangazo katika gazeti la Mzalendo kuhusu nafasi ya kazi ya Udaktari katika hospitali kuu kwenye kaunti yako. Andika barua ya kuomba kazi hiyo na uiambatanishe na tawasifu-kazi yako.
2) Nchini Kenya michezo ya kamari imeharibu vijana wengl sana na inastahili kupigwa marufuku. Jadili
3) Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali ***'Mwenye pupa, hadiriki kula tamu***.
4) Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo……***tangu siku hiyo sijawahi kuuasi ushauri wa wakuu.***

SHULE YA UPILI YA MARANDA

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

MTIHANI WA KIBAADA MWIGO

102/2 KISWAHILI (LUGHA) Karatasi ya 2

Januari — Saa: 2V2

Jina •.....Nambari yaUsajili•.....

Mkondo•.....Sahihi ya mtahiniwa•.....Tarehe• /01/.

Maagizo.

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Andika mkondo wa kidato chako ,tarehe kisha utie sahihi yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali yote.
d) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
e) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
f) Usitoe ukurasa wowote katika kijitabu hiki,
g) Karatasi hii ina kurasa 9 zilizopigwa chapa.
h) Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
	JUMLA	

I. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia

Kitengo cha familia Kimesakamwa na wimbi kali la mabadiliko katika jamii. Namna ambavyo familia zinaendeshwa siku hizi ni tofauti na taratibu za azali. Waama hakuna kipenge cha maisha yetu ambacho hakijaathiriwa na kile ambacho kimekuja kujulikana kama 'usasa'.

Familia nyingi hasa katika maeneo ya mijini zinategemea sana watu wa kuajiri kuzishughulikia. Wazazi wengi hawatengi muda wa kukaa nyumbani na watoto ili kuwapa mwongozo na mapenzi yaliyo muhimu katika hatua mbalimbali za ukuaji wao. Wazazi huondoka mapema sana kwenda kazini na kurejea wakiwa wamechelewa mno. Watoto wao wakati huo huwa ama hawajaamka au tayari washalala. Kwa upande mwingine wapo wazazi ambao wanafanya kazi katika miji iliyo mbali na wanapokaa watoto wao au nchi za kigeni. Uhusiano kati ya mzazi na mtoto unakosa rotuba ya kuuneemesha na matokeo yake huwa ni vijana waliokosa mwelekeo. Walivyosema Waswahili, samaki hukunjwa akiwa bado mbichi. Tabia za watoto hawa zinaweza tu kuandaliwa katika maadili wakiwa wadogo.

Tofauti kati ya wazazi, Pamoja na kuzaliwa kwa watoto nje ya ndoa kumebadilisha sura ya kitengo cha familia. Tofauti na zamani, hii leo utapata familia ambazo zinaendeshwa na mzazi mmoja – anaweza kuwa baba au mama tu. Ni kweli kwamba mtoto huhitaji malezi ya wazazi wote wawili. Mwongozo wa ushirikiano wa wazazi wote wawili ni imara na bora zaidi kuliko wa mzazi mmoja. Hii haimaanishi kuwa mtoto hawezi kulelewa vizuri na mzazi mmoja au vibaya na wazazi wote. Mtoto huweza kukosa huduma za kimsingi kwa kosa lisilo lake.

Jukumu la jamii katika malezi ya watoto limepungua. Zamani malezi ya mtoto yalikuwa jukumu la kila mwanajamii. Mtoto alipothubutu kufanya kosa aliweza kuadhibiwa palepale na mwanajamii yeyote ambaye hakusita kujitwika jukumu la mzazi. Hata hivyo hali ni tofauti hii leo. Kumwadhibu mtoto wa mtu ni kichocheo tosha cha kuleta mfarakano usiokwisha katika jamii. Kila mtu anauchelea ugomvi wa kujitakia. Kila mtoto sasa anaelewa na vipimo vya mzazi wake na siyo vya jamii pana. Watoto nao wamegundua hili na hawakusita kujivika mavazi mawili tofauti, zuri mbele ya wazazi wao na jinginelo popote pasipo hao wazazi. Sasa wazazi wanaweza kuishi na wahalifu waliokubuhu bila kufahamu.

Jambo lingine linalohusiana na hilo ni kutupiliwa mbali kwa tamaduni za Kiafrika. Ni kama jamii iliyotupa jongoo na mti wake. Si siri kuwa kuna masuala ya kitamaduni yaliyopitwa na wakati na ambayo inahalisi kuyapiga teke. Hata hivyo hatuwezi kukitia kila kipengee cha tamaduni zetu jalalani. Utamaduni wetu mbali na kututambulisha kama jamii, pia hutekeleza jukumu adhimu la kutuwezesha kuyaona mambo kwa mtazamo mmoja. Mtazamo huo mmoja ndio unaotupa umoja wetu. Hatuwezi kuwa na utangamano bila kuwa na uzi unaotufunga Pamoja. Maadili ya jamii hayawezi kubainika bila ya watu kuwa na Mwongozo na mtazamo mmoja kuhusu hali yao ya maisha.

Familia za kisasa zina idadi ndogo za watu ikilinganishwa na hapo awali. Hali ngumu ya maisha imewasukuma watu katika kupata watoto wachache ambao wanaweza kumudu kuwalea vizuri. Nako kupungua kwa nafasi za ajira kunawazuia vijana kuingia katika nikahi mapema. Hali hii imechangia katika

kupunguza idadi ya watu na pia kupunguza kasi za uchipukaji wa familia mpya. Hali ngumu ya maisha imepunguza upana wa familia kama ilivyokuwa awali. Siku hizi mtu na mkewe au mumewe Pamoja na watoto wanaikamilisha familia. Vikoa vimekwisha na kubaki kuwa kila mtu na lake. Wengine hawako tayari kuwatilia pondo ndugu zao.

Maswali

1. Kwa mujibu wa taarifa eleza matatizo yanayoweza kuikabili familia inayoendeleshwa na mzazi mmoja. (alama

   2) .....
   .....
   .....

2. Ni nini kiini cha utengano wa wazazi katika ndoa. (alama

   1) .....
   ....

3. Jadili nafasi ya utamaduni katika kuijenga jamii bora kwa kurejelea makala. (alama 2)

   .....
   .....

4. Kwa nini familia za kisasa zina idadi ndogo ya watu? (alama 2)

   .....
   .....
   .....

5. Taja huku ukitoa mifano ya tamathali zozote tatu za lugha zilizotumiwa katika taarifa.(alama 3)

   .....
   .....
   .....
   .....

6. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kifunguni. (alama 5)

i. Kimesakamwa –

.....

ii. Mfarakano usiokwisha

.....

iii. Wahalifu waliokubuhu

.....

iv. Vikoa vimekwisha

.....

v. Kujivika mavazi mawili

.....

2. UFUPISHO

Soma *taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo*

Ki1a walimwengu wanapotajiwa kuwa shambulizi la kigaidi limetokea mahali fulani, wimbi la taharuki huwakumba. Mashambulizi ya kigaidi yameongezeka katika siku za hivi majuzi ambapo kundi Ia watu linalohisi kuwa linaonewa na kukandamizwa huitumia mbinu ya kushambulia kwa kuvizia, hasa kutumia mabomu au kuteka ndege na kutishia kuilipua na wakati mwingine kuilipulia angani. Kuna mabomu yaliyotegwa na kulipuka katika maegesho ya magari au kwenye vizuizi vyamagari. Mengine hutegwa na kulipuliwa katika afisi, mikahawa, makao ya watu, n.k. Katika baadhi ya mashambulizi, wapo waliojitoa mhanga ambao hujilipua katika shambulizi

.

Makundi ya watu wanaohasimiana ndio chanzo cha matendo ya kigaidi. Kundi linalohisi kuwa linaonewa au ambalo kweli linaonewa na ambalo ni dhaifu kuliko lile jingine, hufanya juu chini kushambulia kisirisiri. Nia ni kulipisha kisasi kwa jambo wanalohisi wamehiniwa. Kwa kuwa kundi hilo hudhani kuwa dhaifu halina njia wala uwezo wa kuyakabili moja kwamoja matendo waliyotendewa au wanayoendelea kutendewa, njia ya pekee, kwa maoni yao, huwa hii ya kushambulia kwa kushitukiza. Kiini cha uonevu kinaweza kuwa dini, uchumi, maamuzi ya kisiasa au jambo lingine lolote lile. Kinachobainika katika suala zima Ia mashambulizi ya kigaidi ni kuwa lipo jambo ambalo linazikera nyoyo za kundi fulani Ia watu walio wanyonge ambao huona kuwa njia ya pekee ya kudhihirisha hisia zao ni kupitia mashambulizi ya aina hii.

Mashambulizi ya aina hii yana athari zake nyingi. Kuna watu wanaouawa na wengine wengi kulemaa. Maisha ya watu hawa au jamaa zao wanaowategemea hubadilika na kujaa mvurugano uliokithiri. Kuna watoto ambao ndoto zao zakupata elimu zimetumbukia nyongo baada ya wazazi wao kuzikwa hai katika vifusi. Mbali na kukosa elimu na mahitaji mengine ya kimsingi, watoto hawa hupatwa na matatizo ya kisaikolojia baada ya kuona maafa yaliyowafika wavyele wao. Hata wale wanaosalimika kutoka kwenye vifusi hivi hawaishi kuandamwa na majinamizi yasiyoisha.

Mashambulizi ya kigaidi hayaathiri tu watu pamoja na kuharibu mali ya thamani ya lukuki ya pesa. Zipo athari nyingine hasi ambazo hudhihiri. Kwa mfano usalama wa nchi huwa mashakani. Wananchi na wageni vilevile hujihisi kuwa dhaifu na dhalili katika nchi illyovamiwa. Serikali husika hujikuta katika shutuma kwa kushindwa kutambua mipango hiyo mapema na kuzuia hasara ya nyoyo na mali. Aidha, jamii ya kimataifa huiona nchi hiyo kama yenye kukosa usalama na hivyo kuwaonya raia wake dhidi ya kuizuru. Iwapo nchi husika inategemea utalii kama kitega uchumi muhimu, basi hukosa wateja na waajiriwa katika sekta hii kupigwa kalamu.

Tatizo la ugaidi si Ia nchi moja au mataifa fulani mahususi wala hakuna nchi au taifa linaloweza kudai kuwa haliwezi kukabiliwa na tishio la kigaidi. Kuanzia Dar es Salaam, Nairobi hadi New York na London au hata Cairo hadi Riyadh na Baghdad, sote tunakabiliwa na tatizo hili hili. Hakuna ajuaye lini, vipi au wapi magaidi wamedhamiria kutekeleza unyama huu.

Labda swali Ia kujiuliza ni kwamba; Je, upo uwezekano wa mwenendo huu wa kuwaangamiza watu, wengi wa wahasiriwa wakiwa wale wasio na hatia, kudhibitiwa na kumalizwa kabisa? Serikali za nchi mbalimbali zimejaribu kutumia uwezo wao wa kiuchumi na kiteknolojia ili kujaribu kuiondoa hali hii. Njia waliyoitumia ni ya mtutu wa bunduki ambapo makombora mazito yaliyogharimu pesa nyingi yanadondoshwa katika makao ya washukiwa. Hata katika hatua hii nayo, upo uwezekano mkubwa wa kuuawa watu wasio na hatia vilevile. Pia ni wazi kwamba uhasama unalipwa kwa uhasama na matokeo yake ni ulipizaji kisasi usioisha. Amani inakuwa nadra.
Juhudi za ulimwengu kulaani vitendo hivi ni nzuri ila hazitoshi. Utumiaji nguvu kutafuta ufumbuzi wa kitendawili hiki si suluhisho. Kama wanavyoeleza wanasosholojia, kila kitendo kina sababu zake zilizofichama. Sababu hizo ndizo kichocheo cha vitendo vinavyojidhihiri. Hivyo basi jukumu lipo katika kutambua vichochezi vya mashambulizi na kujitahidi kuvitatua kwa njia ya mashauriano yaliyojengwa katika nia safi ya kuleta usawa na usalama duniani.

Wapo watu wanaoona kuwa vitendo vya mataifa yaliyoendelea kwa nchi changa ndivyo kilele cha ugaidi. Watu wanaona kuwa tabia ya mataifa hayo yenye uwezo kiuchumi na kiteknolojia kuamua na kudhibiti sera na imani za nchi changa ni ugaidi uliokubuhu. Vikwazo hivi huwaacha viongozi hoi na wananchi kuteseka kufuatia ulazimishaji wa sera za kiuchumi na kisiasa zisizohusiana na mahitaji ya watu wa nchi husika wala kuambatana na mahjtajj ya nchi hizi. Hii ni hali inayoyatia mataifa yanayoendelea katika wasiwasi usioisha kutokana na dhiki zisizoisha kusababishwa na mataifa ya kigeni.

II. UFUPISHO

a) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 80, fupisha aya ya pili, tatu na nne. (alama 10)
alama1,mtiririko

b) Eleza njia zinazotumiwa na mataifa ulimwenguni kupambana na ugaidi. (Maneno 40) alama 5; 1 ya mtiririko

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) i.Taja vigezo viwili vya kuanisha irabu. (alama 1)

.....

.....

.....

ii.Tofautisha sauti zifuatazo.(alama.2)

a. /a/ na /i/

b. /e/ na /o/

(b) Ainisha aina za vivumishi katika sentensi ifuatayo.(alama. 2)

Mwalimu mzee alitufundisha vizuri ile mada ngumu.

.....

i.Eleza maana ya kirai. (alama.1)

……

……

ii. Tunga sentensi iliyo na kirai kivumishi na kirai nomino chenye muundo wa W+ V (alama 1)

……

(c) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia "O" rejeshi. (alama 2)

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

……

……

(d) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika hali ya udogo wingi.

Kono lake lilivimba baada ya kuumwa na jibwa. (alama 2)

.....

.....

(e) Tunga sentensi iliyo:(alama 3)

Kitenzi kishirikishi kikamilifu

.....

Kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi

.....

Kiwakilishi cha nafsi ya tatu tegemezi wingi.

.....

(f) Kanusha sentensi ifuatayo kisha ueleze maana yake katika hali kanushi (alama 2)

Angeongoza darasa lake, angepewa tuzo.

.....

.....

.....

(g) Onyesha sehemu za kisarufi katika neno lifuatalo. (alama 2)

Kililiwa

.....

.....

(h) Kanusha katika hali timilifu wakati uliopita.

Kamati ya uchaguzi iliandaa ripoti kuhusu utovu wa nidhamu shuleni.(alama 2)

(i) Changanua kwa kutumia mchoro wa matawi

Hatukuondoka na yeye japo tulirudi naye. (alama 4)

(j) Tumia kiambishi KA katika sentensi ili kuleta dhana ya: (alama 2)

i. Wakati usiodhihirika

.....

ii. Kuonyesha matokeo yanayosababishwa na kitendo.

.....

(k) Chane kwa mtama_____ kwa udongo. (alama 1)

(l) a. Eleza maana ya fungu tenzi. (alama 1)

.....

b.Taja aina mbili za fungu tenzi.(alama.2)

.....

Geuza sentensi hii hadi usemi halisi.

Wanakijiji walikuwa wanataka kujua iwapo vipakatalishi vya shule za msingi vingeweza kuinua kiwango cha elimu. (alama 3)

.....

.....

(m)a. Eleza maana ya yambwa.(alama 1)

.....

b. Tunga sentensi iliyo na: shamirisho kipozi na chagizo cha kiasi kamili. (alama.2)

.....

(n) Tunga sentensi kwa kutumia kiunganishi cha wakati.(alama 2)

.....

(o) Andika visawe vya maneno yaliyopigigwa mstari. (alama 2)

Tulienda <u>kusali</u> siku ya <u>Jumapili.</u>

.....

SWALI LA 4: ISIMU JAMII

Eleza changamoto zinazokumba ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (alama 10)

SHULE YA UPILI YA MARANDA

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

MTIHANI WA KIBAADA MWIGO

102/2 KISWAHILI (LUGHA) Karatasi ya 3

Januari — Saa: 2V2

Jina……Nambari ya mtahiniwa……

Sahihi……Tarehe……

Maagizo

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali **manne** pekee .*
d) *Swali la **kwanza** ni la **lazima.***
e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne. zilizobaki;yaani:Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi.*
f) *Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.*
g) *Majibu yote **lazima** yaadikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
h) Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa.
i) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
	JUMLA	

SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

1.Lazima

a) ”Mwanangu nakuomba uzingatie uadilifu maishani uongofu ni nuru ya mustakabali wa kila mtu…”

i)Tambua kipera na utanzu wa tungo hili (al. 2)

ii)Kwa kutumia hoja **mbili** eleza muundo wa kipera hiki (al. 2)

iii)Fafanua sifa **nane** za kipera hiki (al.8)

b) Eleza vikwazo **vinane** vya ukuaji wa fasihi simulizi. (al.8)

SEHEMU B: RIWAYA

Assumpata k. matei: : chozi la Heri

Jibu swali la 2 au la 3

2.”Si kufua, si kupiga deki, si kupika…almuradi kila siku na adha”

a) a) Eleza muktadha wa kauli hii. (ala.4)

b) Taja mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. (al.2)

c) Kwa kutumia hoja **kumi na nne**, eleza maudhui yaliyodokezwa na dondoo hili. (al.14)

3.”Kila mara hujiuliza ikiwa watoto huwa na hadhi tofauti nje au ndani ya ndoa”

Amali inayotajwa imekumbwa na changamoto chungu nzima.Jadili kwa kurejelea riwaya nzima. (al.20)

SEHEMU C: TAMTHILIA

P. Kea : Kigogo

Jibu swali la 4 au la 5

4.”Acha porojo zako. Kigogo hachezewi;watafuta maangamizi!”

a)Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)

b)Fafanua sifa za mzungumzaji (al.6)

c)Kwa kurejelea hoja **kum**i, thibitisha kwamba kucheza na kigogo anayerejewa ni sawa na kutafuta maangamizi (al.10)

5.”Tunahitaji kuandika historia yetu upya.”

a)Eleza sababu **kumi na mbili** kuonyesha kwa nini ilikuwa muhimu kuiandika historia ya sagamoyo upya (al.12)

b)Onyesha mikakati inayotumiwa kuiandika upya historia ya Jumuiya ya sagamoyo (al.8)

SEHEMU D: USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

6.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

LONGA

Longa longea afwaji, watabusarika

Longa uwape noleji, watanusurika
Longa nenea mabubu,sema na viduko

Longa usichachawizwe, tamka maneno
Longa usitatanizwe, mbwa aso meno
Longa usidakihizwe,kishindo cha funo

Longa yote si uasi, si tenge si noma
Longa pasi wasiwasi,ongea kalima
Longa ukuli kwa kasi, likate mtima

Longa zungumza basi, liume ja uma
Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa
Longa liume wakora, kwani wezi miwa

Longa bangu na parara, hawakuitiwa
Longa bunge si kiwara, si medani tawa
Longa ni simba marara, wanaturaruwa.

Maswali

a) Tambua na ueleze nafsi neni katika shairi hili (al.1)
b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kilivyotumika kukidhi mahitaji ya kiarudhi (al.4)
c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari **nne** zilizotumika na mtunzi kwenye shairi hili. (al.4)
d) Eleza aina **tatu** za urudiaji katika shairi (al.3)
e) Tambua na ueleze **ton**i ya shairi (al.2)
f) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi. (al.2)
   i. Afwaji
   ii. Tenge
g) Eleza umbo la shairi hili. (al.4)

7.**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Kila nikaapo husikia tama
Na kuwazia hali inayonizunguka

Huyawazia madhila
Huziwazia shida
Hujiwazia dhiki

Dhiki ya ulezi
Shida ya kudhalilishwa kazini
Madhila ya kufanyiwa dharau
Kwa sababu jinsia ya kike
Hukaa na kujidadisi

Hujidadisi kujua ni kwa nini
Jamii haikisikii kilio changu
Wezangu hawanishiki mikono
Bali wananidharau kwa kuikosea utamaduni

Hukaa na kujiuliza
Iwapi raha yangu ulimwengu huu?
Iwapi jamaa nzimaa ya wanawake?

Maswali

a) Taja sifa **mbili** za shairi huru zinazojitokeza katika shairi hili (al.2)
b) Eleza dhamira ya mshairi (al.2)
c) Kwa kutoa mifano, eleza maana ya mistari mishata (al.3)
d) Bainisha tamathali **mbil**i za usemi zilizotumika katika shairi hili (al.4)
e) Eleza nafsineni katika shairi hiri (al.2)
f) Tambua **toni** ya shairi hili (al.2)
g) Taja maudhui **matatu** katika shairi hili (al.3)
h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi (al.2)
   Madhila
   Kudhalilishwa

SEHEMU E: HADITHI FUPI

A. Chokocho na D kayanda : Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine.

8."…hamna mwendawazimu wala mahoka kati yetu, mimi nimepewa zawadi hizo"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
b) Eleza sifa nne za msemaji (al.4)
c) Hakiki nafasi ya maudhui ya busara kwa mujibu wa hadithi hii (al.12)

SHULE YA UPILI YA KITAIFA YA KAPSABET

Kenya Certificate of Secondary Education

MTIHANI WA MWIGO

102/1 — KISWAHILI —Karatasi ya 1 INSHA

.—Muda: Saa 1$_{3/4}$

_____

Jina…….Nambari ya Usajili……..

Mkondo…….Tarehe……

Maagizo

a) Andika jina lako,nambari ya usajili, mkondo katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
*b) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima**.*
c) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.
*d) Kila insha isipungue maneno **400.***
e) Kila insha ni alama 20.
f) Kila insha ni lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
*g) Insha zote **sharti** ziandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*h) **Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa.***
*i) **Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

1. **Lazima**

   Wewe ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Upili ya Mamboleo. Mwanafunzi wako aliyefanya mtihani wake wa KSCE mwaka jana na kupita vizuri amepewa nafasi katika Chuo Kikuu cha Tumaini. Andika wasifu wake.

2. Mitandao ya kijamii ina faida na hasara zake. Thibitisha.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

   Wakosanao ndio wapatanao.

4. Andika kisa kinachomalizikia kwa kauli ifuatayo:

…Tangu siku hiyo kijiji kizima kilipata funzo kwamba umdhaniaye ndiye kumbe siye na umdhaniaye siye kumbe ndiye.\

SHULE YA UPILI YA KAPSABET

KISWAHILI KIDATO CHA NNE

Ufahamu, Ufupisho Sarufi na Matumizi ya Lugha, Isimu-jamii

MTIHANI WA MWISHO WA MIHULA WA PILI

Jina: …… ..

Darasa: ……..... *Nambari ya usajili:* ……..

Sahihi: …….. *Tarehe:* ……..

Maagizo

(a) Andika **jina** lako, **darasa** na **nambari** yako ya usajili (Adm.).
(b) Tia **sahihi** yako kisha uandike **tarehe** ya leo
(c) Jibu maswali **yote**
(d) **Majibu** yako yaandikwe katika **nafasi** ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
(e) Majibu yote lazima yaandikwe katika **lugha ya Kiswahili**.
(f) **Usitoe ukurasa** wowote kutoka kwenye kijitabu hiki
(g) Karatasi hii ina **kurasa 10** zilizopigwa chapa
(h) Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote **zimepigwa chapa** na kuwa maswali yote yamo

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	*Upeo*	*Alama*
1.	15	
2.	15	
3.	40	
4.	10	
Jumla	**80**	

Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Mbuga ya Ziwa Nakuru, sasa imesafishwa katika mojawapo ya juhudi za kukabiliana na maji taka yanayoingia mbugani. Wasimamizi wa mbuga walitumia huduma za vijana wasiokuwa na ajira kutoka mitaa ya Bondeni, Kivumbini, Lake view, Free area na Flamingo kusafisha mito inayobeba uchafu huo.

Vibarua walizoa jumla ya tani 1.5, na baadaye tani 4.2 idadi inayofikisha zaidi ya tani 6.0 kwa siku mbili mfululizo.Hili linaashiria jinsi kina cha uchafuzi wa mazingira kwenye ziwa Nakuru umeshamiri,na baadhi ya wafanyikazi wanaona litajwe kuwa janga la kitaifa linalokodolea macho mbuga nyingi humu nchini.

Shughuli hiyo ilivutia hisia mseto huku maswali mengi kuliko majibu yakiibuka, endapo KWS ina bajeti ya kung'arisha mbuga za wanyama.

Akizungumza na *Taifa Leo,* mwangalizi wa utalii kutoka mbuga ya wanyama ya Ziwa Nakuru Bw Sirman Kioko, alisema maji taka yamekuwa yakiingia kwenye mbuga kutokana na miundo msingi duni. Aliongezea kuwa maisha ya wanyama hasa simba, nyati, vifaru, chui, viboko na flamingo yalikuwa hatarini,kwa sababu ya maji taka yalikuwa yamebadili mkondo na kupenyeza kwenye mbuga.

Miaka mitano iliyopita mbuga ya Nakuru ilikuwa na idadi kubwa ya ndege aina ya heroe ,lakini sasa wamebakia 200 tu. Hali hii itazidi kuwa mbaya,endapo idara husika haitaweka mikakati ya kutafuta suluhu la kudumu kwa wanyama pori wanaozidi kuangamia. Aidha uchafuzi katika ziwa Nakuru umefanya ndege kuhamia ziwa Bogoria ambapo inaaminika angalau chakula ni tele.

"Tunakubali kuwa gharama ya kusafisha mbuga ni kubwa,lakini pia tunaomba umma kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki inayoziba njia za maji,"alisema.

Pia aliongezea kuwa ni jukumu la mbuga kusafisha mazingira ya wanyama,lakini baraza la mji wa Nakuru pia lina nafasi kubwa ya kuhakikisha makazi ya watu ni safi,kwa kuzoa taka ipasavyo. Anaona kuna utepetevu mkubwa kutoka kwa usimamizi wa mazingira NEMA,wanaostahili kuweka sheria kali za kukabiliana na wale wanaoharibu mazingira.

Aliongezea kuwa baraza la kusimamia huduma za wanyama pori (KWS),halina bajeti ya kusafisha mbuga na ndio sababu waliwaajiri vibarua saba kuendesha shughuli hiyo ya siku tatu. Uchafuzi wa mito inayoingia ziwa Nakuru hutokea msimu wa mvua ambapo maji hufurika na kusomba taka kutoka kwenye makazi ya watu.

Wanyama wanaovutia watalii kama vile Nyati hupata maradhi pindi wanapokunywa maji chafu,yaliyochanganyika na mifuko ya plastiki. Licha ya KWS kumiliki kituo cha kufanyia utafiti aina ya maradhi mbalimbali yanayokabili wanyama bado hawajafanikiwa kwa asilimia kubwa kuyazuia.

Hili linajiri siku moja tu baada ya wakazi wa mtaa wa Bondeni kuandamana barabarani wakilalamikia,ongezeko la kiwango cha takataka kwenye makazi ya watu.

(Imenukuliwa kutoka kwa Gazeti la *Taifa Leo*)

Maswali

1. Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (alama 1)

   ……

2. Eleza sababu zinazofanya Ziwa Nakuru kuchafuka. (alama 2)

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……

3. Ni nini madhara ya kuchafuliwa kwa Ziwa Nakuru? (alama 4)

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……

4. Eleza vizingiti vinavyofanya ziwa hili kuendelea kuchafuliwa. (alama 2)

   ……

   ……

   ……

5. Toa mapendekezo yanayoweza kusaidia kumaliza uchafuzi wa Ziwa Nakuru kulingana na taarifa hii. (alama 4)

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……..…….

6. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika taarifa. **(alama 2)** a. Kupenyeza

…… b.

Utepetevu

……

2. **UFUPISHO (ALAMA 15)**

Sekta ya kilimo nchini Kenya ni mojawapo ya mihimili ya uchumi na inachangia asilimia 25 ya pato la taifa (G.D.P.). Sekta hii inatoa ajira kwa asilimia 40 ya wakenya na zaidi ya asilimia 70 ya wanaoishi mashambani. Isitoshe, huchangia asilimia 65 ya mapato yanayotokana na mauzo ya nje ya nchi sawa na kutegemewa na zaidi ya asilimia 80 ya wakenya wote kwa uhai wao kupitia kutoa ajira, ujira na usalama wa chakula. Nchini Kenya, kilimo kinakumbwa na changamoto na vitisho kama vile kupanda kwa gharama ya kawi, kubadilika kwa tabia ya nchi pamoja na misukosuko katika nchi jirani. Bila shaka kumarika kwa sekta hii kutahakikisha kustawi kwa uchumi mzima. Hivyo basi, sera na mifumo ya kiasisi inayosimamia sekta hii ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wote.

Ili kuwakinga wanunuzi dhidi ya tishio la usalama wa chakula, serikali imetekeleza maamuzi mengi katika sekta ya kilimo. Kutokana na hali hii mbinu za kuusitiri umma zimepewa kipaumbele katika sera za nchi. Pamoja na hayo, sera za bei za bidhaa za kilimo, zenye kuwafaidi wazalishaji, nazo katika miaka ya hivi karibuni zimebainishwa na kushiriki kikamilifu pamoja na udhibiti wa serikali; ambayo miongoni mwa mengine, huamua bei za bidhaa zinazozalishwa pamoja na pembejeo. Kuhusu hifadhi ya nafaka, mnamo 2011 Kenya ilipanga kuongeza maradufu hifadhi hii ili kujikinga dhidi ya upungufu wa chakula kufuatia utabiri kuwa mvua imepungua.

Baada ya kuukinga umma kutokana na athari za njaa, serikali ilielekeza juhudi zake kwenye hatua za kibiashara. Kufuatia upungufu wa chakula kumekuwa na juhudi za kupunguza ushuru wa uagizaji hasa wa mahindi, mchele na sukari. Sambamba na hayo, Kenya imekuwa ikiongeza hisa inayotengea Wizara ya Kilimo kufikia asilimia 10 ya jumla ya makadirio yake ya fedha ili kuafiki Azimio la Mapato linalosisitiza serikali zote kutenda hivyo.

<u>Maswali:</u>

a) Kwa maneno 35 – 40 fupisha aya ya kwanza ya kifungu hiki. (alama 6, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

.....

b) Kwa maneno 50-55, fafanua mikakati iliyochukuliwa na serikali ya Kenya ili kuimarisha kilimo. (alama 9, 1 utiririko) Matayarisho

.....

3. **MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)**

a) Taja ala zinazotumika kutamkia sauti /ch/ (alama 1)

.....

.....

b) Tunga sentensi moja ukitumia nomino na kielezi kutokana na neno: enda (alama 2)

.....

.....

c) Tunga sentensi ukitumia nomino katika ngeli ya 'U-YA' ili kuonyesha upatanisho wa kisarufi (alama 2)

.....

.....

d) Eleza tofauti za sentensi hizi. (alama 2)

i. Nilimpata huku.

ii. Nilimpata humu.

.....

.....

e) Onyesha matumizi ya kiambishi 'ji' katika sentensi ifuatayo:
Mkiambiaji alijibidiisha katika riadha (alama 2)

.....

.....

f) Tumia vitenzi vifuatavyo kutunga sentensi katika kauli ya kutendeka

(i) Cha (alama 1)

.....

.....

(ii) Pa (alama 1)

.....

.....

g) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao KN(N) + KT (t + T + E) (alama 1)

.....

.....

h) Tumia neno *'Kama'* katika sentensi kama; (alama 2) i. Kitenzi

……

……

ii. Kihusishi

.....

i) Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi cha uteuzi (alama 2)

.....

.....

j) i) Kirai ni nini? (alama 1)

.....

.....

ii) Onyesha aina ya virai katika sentensi ifuatayo.
Mwaka juzi alikwenda ulaya (alama 2)

....

.....

.....

k) Kwa kutoa mfano mmoja wa sentensi eleza maana ya shamirisho kitondo (alama 2)

.....

.....

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi: (alama 4)
Ule mkongojo wa babu ulinunuliwa na fundi

.....

....

....

....

.....

....

....

....

....

.....

.....

m) Tunga sentensi moja ukitumia vitate hivi: (alama 3) (i) Kipofu

.....

(ii) Kibovu

.....

(iii) Kibofu

.....

n) Eleza mofimu zilizomo katika neno hili. (alama 3)
Lililolila

....

.....

.....

.....

o) Tunga sentensi moja ukitumia kihisishi cha masikitiko. (alama 2)

.....

.....

p) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya alama ya kibainishi. (alama 2)

.....

.....

q) Andika katika usemi wa taarifa
"Utaweza kuwa mwindaji mashuhuri ikiwa utayafuata mashauri yangu,"
alisema mbunda. (alama 2)

.....

.....

.....

r) Tunga sentensi ukitumia kinyume cha kitenzi hiki: Ezeka (alama 2)

.....

..... s)

Yakinisha sentensi ifuatayo:

Tusingalienda hospitali, tusingalitibiwa. (alama 1)

.....

.....

4. **ISIMU JAMII: (ALAMA 10)**

a) Fafanua istilahi zifuatazo za isimu jamii (alama 2) (i) Isimu

.....

.....

.....

(ii) Jamii

.....

.....

.....

b) ".....ah.....naomba kumwongelesha Chucho.....Naam, naam Chucho.....Hujambo? .....si.....sina neno.....naam. Mjomba amezidiwa si wa maji si wa chakula....kweli?.....Muuguzi mkuu amedhihirisha..... Yes.....ok.....yeah.....Ala! Ameishiwa na pesa.

(i) Tambua sajili husika katika dondoo hili. (alama 1)

.....

.....

(ii) Kwa hoja zozote saba, eleza sifa za sajili hii. (alama 7)

.....

.....

.....

.....

KCSE / MOCK EXAMINATIONS

102/3 - KISWAHILI - Karatasi ya 3 FASIHI

Muda: Saa 2½

Jina..... Nambari ya Mtahiniwa .....

Sahihi.....Tarehe:../12/ KIDATO 4...

KAPSABET HIGH SCHOOL

Maagizo

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
*(c) Jibu maswali **manne** pekee.*
*(d) Swali la kwanza ni la **lazima.***
(e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani:Riwaya, Ushairi,Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi
*(f) Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.*
(g) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(h) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizotengewa kwenye kijitabu hiki cha maswali.
*(i) Kijitabu hiki kina kurasa **tano** zilizopigwa chapa.*
(j) Mtahiniwa ni lazima ahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa na maswali yote yamo.

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	

SEHEMU A: TAMTHILIA P. Kea: *Kigogo*

1. **LAZIMA**

"...binadamu ni mavumbi na mavumbi atarejea kwa maana, kwa tamaa mtu anapenda kula kuku huku nduguze wakila kama kuku. Na katika uchu huo huo amependa kufikia kilele cha ufanisi kwa kukanyaga migongo ya wenziwe...

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4) (b) Kwa kutoa mifano **mitatu** katika dondoo hili, ainisha taswira zinazojitokeza. (alama 6)

(c) Huku ukitoa mifano **kumi**, jadili namna Wanasagamoyo walilemaza juhudi zao za kujikomboa. (alama 10)

SEHEMU B: RIWAYA

Matei: *Chozi la Heri*

Jibu swali la 2 au 3

2. "Barafu iliyokuwa imegandia moyoni ilianza kuyeyuka na moyo kutwaa uvuguvugu. Hatimaye uyabisi wa moyo wake ulitoweka."

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Taja na ueleze sifa sita za mrejelewa. (alama 6)
(c) Jadili maudhui yanayobainika katika dondoo hili. (alama 10)

AU

3. "Mama mtu alikuwa ameamua kwamba hapa hapamweki. Alikuwa amehudumu katika afisi za umma kama mhazili mwandamizi kwa miaka mingi mpaka kazi hii akaiona inamfanya kusinyaa, hana hamu tena."

(a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza riwaya ya Chozi la Heri. (alama 6)
(b) Huku ukitoa mifano jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa kwa mujibu wa riwaya hii. (alama 14)

SEHEMU C: USHAIRI

Jibu swali la 4 au 5

4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Ningeuzwa kuchaguwa, mambo nisiyo yapenda Pasipo na kuchelewa,
ningeanza na kukonda
Kujapo kwa kuuguwa, kunilaza kwa kitanda

Ningeishutumu njaa, kama adui mkuu Aso na fao
kufaa, mwana wala mjukuu Mtu hapati kukaa, hatui
ya juujuu.

Kisha ningetaja vita, nduli ya tangu zamani
Fundi wa vyembe na nyuta, si mwema simtamani
Ni mtu wa vutavuta, kamwa hapendi amani

Na katika mlolongo, kwenye huu msururu Ningetaja na
kifungo, kutokuwa na uhuru Heri kwangu kuwa chongo,
itakuwa haidhuru.

Kadhalika na ukata, ningasahau siwezi
Hauna pato kupata, kuyakidhi matumizi
Hana haramu mkata, dawamu ya muombezi

Ninguelani ukuwa, pamwe na athari zake
Nijapo kuvunjikiwa, ukanikuta upweke
Ni kama madhila huwa, una dhiki ndani yake

Na mishale kama hiyo, ifumayo moyo wangu
Inganipa jakamoyo, siyo matilaba yangu
Ngawa siridhiki kwayo, ni kudura zake Mungu

Maswali

(i) Eleza mambo ambayo nafsi neni hayapendi na kwa nini? (alama 5)

(ii) Kwa kurejelea shairi hili, eleza umuhimu wa: (alama 6)

(a) inkisari
(b) tabdila
(c) kufinyanga sarufi

(iii) Ainisha bahari tatu za mashairi ukirejelea shairi hili. (alama 3)

(iv) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 3)

(v) Eleza mbinu tatu ambazo zimetumiwa kusanifu ubeti wa tatu. (alama 3)

AU 5. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Bustani za jadi
Maua ya kuchezea vipepeo
Na pua kufurahisha
Sasa ni mabaki ya kumbukumbu
Za yaliyojiri hapa
Na kukiacha kijiji kinywa wazi.

Hapa walimpiga mwereka
Dada yangu; mdogo wangu
Shuleni akitoka
Na mkoba wa kilo nzito za vitabu Chini
akakandamiziwa Wakachana mbuga na wake
ubikira!

Pale kando ya mto
Walimvizia na kumburura shangazi
Binamu zangu wadogo wakiona
Marinda wakamchania

Kabla ya kumtia kidonda shangazi Naye ami kumchania kovu moyoni!

Ni hapa kando ya barabara kuu
Ambapo nyanyangu walimshika mkono
Uchochoroni wakamburuta
Na kumfanya kujutia
Bahati mbaya ya kuishi kwingi
Akaganda uchochoroni Hadi alipoletwa nyumbani kesho yake Na wachungaji wa machungani.

Si hapa walipomshurutisha mama
Chini wakamkanyagia
Kama kuku wa kuchinja
Baada ya yake sidiria kuikata?
Si hapa sebuleni mwetu?

Si hapa sokoni
Nilipopata vazi la stara
La wangu mke mpendwa Lililokatwa yake mihimili?
Yule kichaa wa mwetu sokoni.
Akawa kichwani amelivaa
Na kuimba wimbo wa maombolezi Huku wanakijiji wakimpuuza Na watoto kumcheka?

Ni hapa ambapo usiku ulipoingia
Hawakusita kuhakikisha kuwa
Yule kichaa amawazalia mtoto Na kujitia kundini kushangaa Kilichomtuma atake kujifungua!

(*Timothy Arege)*

Maswali

(a) Tambulisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)
(b) Eleza dhamina ya mshairi. (alama2)
(c) Fafanua mbinu za kimtindo zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 5)
(d) Bainisha aina za taswira katika shairi hili. (alama 4)
(e) Onyesha toni ya mshairi. (alama 2)
(f) Onyesha matumizi ya mishata katika shairi hili. (alama 1)
(g) Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 4)

SEHEMU D: HADITHI FUPI

Jibu swali la 6 au 7

A.Chokocho na D. Kayanda (Wah): *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

6. ***D. Kayanda*: "Mwalimu Mstaafu"**

"Watu wa kwetu husema, 'Usilipe jema kwa baya', kwa hiyo mimi ninacho changu ambacho nitakupa kwa hiari yangu mwenyewe..."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) 'Usilipe jema kwa baya'. Fafanua kinaya katika kauli hii kwa kurejelea hadithi ya 'Mwalimu Mstaafu". (alama 16)

AU

7. ***Mtihani Wa Maisha (Eunice Kimaliro)***

(a) "Labda hata tayari ameona maajabu niliyoyafanya kwenye mtihani. Atanipa hongera kabla ya kunipa matokeo".

(i) Eleza mbinu kuu ya kimtindo katika dondoo hili. (alama 2)

(ii) Fananua umuhimu wa msemaji wa dondoo hili ukirejelea hadithi ya "Mtihani wa Maisha". (alama 6)

(b) *S. O. Hamad*: "Shibe Inatumaliza"

"Ndugu yangu **<u>kula kunatumaliza</u>**."
"Kunatumaliza au tunakumaliza?"
Jadili ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kutoa mifano kwenye hadithi.

(alama 12)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Kila kukicha mashaka
Ni kero hili si huba
Mimi pendo la viraka, heri demu la mkoba
Ingawa mno nataka, kuishi nawe muhiba
Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

Kamwe sitoshughulika
Nawaje wenye kuziba
Viumbe wanosifika, kwa fedha, chuma na shaba
Walostarabika, si mimi wa tobatoba
Pendo viraka viraka

Litanishinda kuziba

Naapa sitojitweka
Limenichosha si haba
Nasomba vyangu viraka, nitie kwenye mkoba
Sikuye ya kuzinduka, mjinga hawi ni juba
Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

(a) Huu ni wimbo wa mapenzi. Thibitisha. (alama 2)
(b) Eleza sifa tatu za nafsinenewa katika wimbo huu. (alama 3) (c) Fafanua mbinu nne ambazo nafsineni ametumia kufanikisha uwasilishaji wake. (alama 4)
(d) Eleza faida tano za kurithisha wimbo huu kwa vizazi vijavyo. (alama 5)
(e) Unanuia kufanya utafiti kuhusu utungo wa maigizo:-
(i) Eleza hatua tatu utakazofuata katika utafiti wa utungo huu. (alama 3)
(ii) Fafanua udhaifu wa kuhifadhi utungo huu kwa njia ya maandishi. (alama 3)

MTIHANI WA PEAK

MUHULA WA TATU- JANUARI
KIDATO CHA NNE – KISWAHILI KARATASI YA 1

102/1
KISWAHILI
Karatasiya 1
INSHA
MUDA: SAA 1 ¾

JINA _____ NAMBARI_____

SAHIHI _____ TAREHE_____

DARASA_____

Kwa matumizi ya mtahini pekee

SWALI	UPEO	UMEPATA
1	**20**	
2	**20**	
JUMLA	**40**	

1. Andika barua kwa mhariri wagazeti la ‘Sanifisha’ ukitoa maoni yako kuhusu jinsi yakuendeleza utangamano wa kitaifa.
2. Jadili matatizo yanayowakumba vijana katika jamii ya leo.

3. Ibilisi wa mtu ni mtu.
4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo.

   “Nilipowakumbuka wenzangu, macho yaliingia kiwi, machozi ya kanilengalenga……”

MTIHANI WA PEAK
MUHULA WA TATU - JANUARI
KIDATO CHA NNE – KISWAHILI KARATASI YA 2

102/2
KISWAHILI
LUGHA
Karatasi ya 2
Muda: Saa $2\frac{1}{2}$

JINA _____ NAMBARI_____

SAHIHI _____ TAREHE_____

DARASA_____

Maagizo

a) Andika jina lako, nambari ya usajili na darasa lako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
*b) Jibu maswali **yote** katika nafasi ulizopewa.*
c) Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

Swali	**Upeo**	**Alama**
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	**80**	

SEHEMU YA A- UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha jibu maswali

Zaraa ndio uti wa mgongo wa taifa Ia Kenya. Viwanda vingi nchini hutegemea kilimo kama malighafi na kuwalisha wafanyakazi. Licha ya umuhimu wa sekta hii, mkulima ambaye ndiye nguzo ya zaraa anaende lea kukabiliwa na matatizo mbalimbali yanayokwamiza juhudi zake.

Mojawapo ya matatizo yanayomkabili mkulima ni ukosefu wa ushauri wa zaraa. Wataalamu wanaotarajiwa kumshauri mkulima kuhusu njia bora za kuzalisha na kuongeza pato lake ni haba ikilinganishwa na idadi ya wakulima wanaohitaji ushauri. Wachache walioko nao wanakwamizwa na mambo tofauti. Mathalani, utawapata hawaendi nyanjani ili kukutana na wakulima kwa kuwa hawana vyombo vya usafiri. Iwapo vipo, huenda petroli ikawa ni kizungumkuti Halikadhalika, usisahau kuwa baadhi ya wataalamu hawa ni walazadamu au mafisadi. Kuna wale wanaofika ofisini na kushinda siku nzima wakisoma gazeti huku wakijaza miraba, wakicheza bao au karata. Kuna wale nao ambao hufika ofisini wakaangika koti au sweta kitini ili waonekane kuwa bado wapo na kisha kutokomea kwenda kushughulikia mambo yao ya kibinafsi yasiyohusu ndewe wala sikio kazi waliyoajiriwa kuifanya.

Ukosefu wa sera mwafaka kuhusu ardhi nalo ni tatizo jingine linalotatiza kilimo nchini. Serikali haijaweka sera mahususi kuhusu matumizi ya ardhi. Wananchi wengi huongozwa na taratibu za utamaduni za nasaba zao. Taratibu hizi hupendekeza ugawaji wa ardhi kwa minajili ya urithi kulingana na warithi waliopo. Si ajabu kuwa kote nchini, ardhi inayofaa kwa kilimo imekatwakakatwa vipande vidogovidogo ambavyo haviwezi kuwa na faida kwa zaraa.

Kushindwa kwa mkulima kuongeza virutubishi ardhini ni changamoto nyingine inayokabili kilimo nchini. Ulimaji wa kile kipande cha ardhi mwaka nenda mwaka rudi, bila kukipa nafasi ya kukipumzisha, huufanya mchanga kupoteza virutubishi muhimu vinavyohitajiwa na mimea. Hili nalo huchangia kupunguza uzalishaji wa mazao. Ili kutatua tatizo hili, wakulima wengi hukimbilia mbolea za kisasa ambazo badala ya kumsaidia, humwongezea madhila. Mbolea hizi zinatambulikana kuchangia uchafuzi wa mchanga na ardhi.

Mabadiliko ya hali ya anga nayo huongeza msururu wa madhila ya mkulima. Mabadiliko haya yamemfanya mkulima kushindwa kupanga wakati anaotakiwa kutayarisha shamba, kupanda, kupalilia, kunyunyizia dawa na kadhalika kwa sababu mvua imekuwa adimu. Badala yake panakuwa na vipindi virefu vya kiangazi ambavyo huathiri bidii za mkulima. Maji nayo yanaendelea kupungua na wakulima wengi hawawezi kukimu mahitaji ya unyunyizaji maji mashambani.

Maradhi pamoja na wadudu waharibifu kama vile viwavi, kupena mbung'o ni changamoto nyingine inayotatiza juhudi za mkulima hapa nchini. Haya hupunguza uzalishaji wa mkulima au wakati mwingine kupunguza mifugo au mimea yake.

Kwa sadfa, iwapo mkulima ataweza kuzalisha mazao licha ya msururu huu wa vikwazo; ana tatizo jingine linalomngojea: ukosefu wa soko kwa mazao yake. Aghalabu, maeneo mengi yanayotoa mazao ya kilimo kwa wingi huwa na matatizo ya usafiri. Njia na barabara huwa mbovu na hazipitiki. Mazao mengi huwa hayafiki sokoni kwa wakati na huwa ni hasara kwa wakulima.

Fauka ya hayo, gharama ya uzalishaji wa mazao ya kilimo hapa nchini huwa ya juu zaidi kuliko faida anayopata mkulima. Watu wengi wameacha kutegemea kilimo kama njia ya ajira kwa kuwa hakilipi. Hii ni zaidi ya ushindani wa bidhaa za kilimo kutoka nje ya nchi ambao ni tatizo jingine linalomkabili mkulima. Mara nyingune wakulima wa kutoka nje ya nchi husaidiwa na serikabi zao kuzalisha mazao kwa kufidiwa au kupewa karadha. Mazao kama haya yaingiapo sokoni huuzwa kwa bei ya chini na hayawezi kushindana na yale ya wale wasiopata mchango wowote kutoka kwa serikali kama wakulima wa hapa nchini. Mkulima wa Kenya anahitaji msaada wa dharura ili aweze

kunyanyua kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa uchumi wetu. Lau haya hayatofanyika, uchumi wetu utaendelea kudidimia.

Maswali

(a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. ***(Alama1)***

_____

(b) Kilimo kina umuhimu gani hapa nchini? ***(Alama2)***

_____

_____

(c) Ni kwa nini wataalamu wa kilimo waliopo hawawafai wakulima nyanjani? ***(Alama4)***

_____

(d) Eleza sababu zozote **nne** zinazokinga mkulima kuzalisha mazao ya kutosha. ***(Alama 4)***

_____

_____

(e) Kwa nini watu wengi wameacha kutegemea kilimo kama njia ya ajira ***(Alama 2)***

_____

(f) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika taarifa. ***(Alama 2)***

(i) Walazadamu

(ii) Karadha

_____

_____

_____

SWALA LA 2: UFUPISHO

Ajira ya watoto ni tatizo sugu linalokumba ulimwengu wa sasa, hasa katikanchi zinazoendelea. Jambo la kusikitisha ni kwamba hivi ndivyo ilivyyo katika nchi nyingi za ulimwengu huu. Kuna idadi kubwa ya watoto wanaoajiriwa katika Nyanja mbalimbali za jamii. Zipo sababu nyingi zinazowasukuma watoto kutafuta ajira barani Afrika kwa mfano, familia nyingi huishi maisha ya ufukara hivi kwamba hushindwa kuyatimiza mahitaji muhimu hususan kwa watoto. Kupanda kwa gharama ya maisha kunazidisha viwango vya umaskini. Ukosefu wa lishe pia huwafanya watoto kutoroka nyumbani kutafuta ajira. Janga la UKIMWI limesababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya mayatima wanaoshia kutafuta ajira ili kuyakimu maisha. UKIMWI umezifanya familia nyingi pia kuwaondoa watoto shuleni ili waweze kuajiriwa kwa lengo la kuzalisha pato la familia hizo. Watoto wengine hutoroka makwao kwasababu ya maonevu. Maonevu haya ni kama vile kupigwa, kutukanwa kila wakati, kunyanyaswa kijinsia na kadhalika. Huko nje hutaabishwa kimwili na kiakili. Hufanyishwa kazi za sulubu zenye malipo duni au wasilipwe kabisa. Hili huwasononesha na kuathiri afya yao.

Wengine hujiingiza katika vitendo vya jinai pale wanapokosa ajira. Huchukua sheria mikononomwao, wakaendeleza vitendo vya ukatili kama vile kuwahangaisha watu na kupora mali yao au hata kuwakaba roho. Aidha, wengine hujikuta kwenye madanguro ambako huendesha biashara.

Uundaji wa umoja wa Afrika hivi majuzi ni hatua muhimu ya kushughulikia matatizo ya Afrika kamavile ajira ya watoto, kuzorota kwa miundo msingi, magonjwa, njaa, umaskini, ufisadi na ukabila. Katika kushughulikia haki za watoto, nchi za Afrika hazina budi kuzingatia masharti yaliyowekwa na Umioja na Mataifa kuhusu haki za watoto. Nchi hizi basi lazima zishugulikie haki za watoto kupitia sharia za nchi. Watoto ni rasilmali muhimu na ndio tumaini la kuwepo kwa kizazi cha binadamu.

a) Fupisha ujumbe wa mwandishi katika aya ya kwanza. (Maneno 45-50) (al 7, 1 ya utiririko)

Matayarisho

_____

_____

_____

_____

_____
_____
_____
_____
_____

JIBU

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

b). Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi fupisha aya mbili za mwisho.
(Maneno 50-55) (maneno 8, 1 ya Mtiririko)

Matayarisho

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

JIBU

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) (i) Taja sauti mbili mwambatano ambazo hutamkiwa midomoni. (al 2)

_____
_____

(ii) Taja sauti moja yenye sifa ifuatayo. (al 1)

_____
_____

b) Andika neno moja lenye viambajengo vifuatavyo:

Nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita, yambwa, mzizi, kauli tendesha, kauli tenda (al 3)

_____

_____

c) (i) Shadda ni nini? (al 1)

_____

_____

(ii) Onyesha iliko shadda mara mbili kwenye neno hili na ueleze ili kuleta maana zake mbili tofauti.

a) Barabara

_____

b) Barabara

_____

(al 2)

d) Huku ukitoa mifano eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili. (al 2)

_____

_____

e) Tumia neno 'Kimya' katika sentensi kama:

(i) Kielezi (al 1)

_____

(ii) Kihisishi (al 1)

_____

f) Weka nomino ifuatayo katika ngeli mbili tofauti.

Uwele (al 2)

_____

g) Tumia kirejeshi 'O' katika sentensi ifuatayo.

Mtu ambaye hutupa tope hujichafua mwenyewe. (al 2)

_____

h) Geuza katika usemi wa taarifa.

"Nitaleta kitabu hiki kesho iwapo utakuwepo, "Maria alimwambia rafikiye. (al 3)

_____

i) Onyesha virai katika sentensi ifuatayo.

Moto ule mkali uliziteketeza nyumba zote karibu na mji ule. (al 3)

_____

j) Onyesha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo.

Nyanya alimpikia mjukuu wake uji mtamu kwa unga mweupe. (al 3)

_____

_____

k) Jibu maswali yafuatayo kulingana na maagizo. (al 4)

(i) Ningalikuwa kiongozi ningalileta maendeleo nchini (kanusha)

_____

(ii) Manakaanga haba manapogonjeka. (sahihisha)

_____

(iii) Mzee ule alibeba meza kubwa (udogo, wingi)

_____

_____

(iv) Sijui anakosomeaJuma. Ningeenda kumtembelea (unganisha kwa kiunganishi lau)

_____

l) Eleza matumizi matatu ya neno 'na' katika sentensi ifuatayo.

Amina na Juma wanasema eti nyumba yao ilijengwa na mwashi hodari. (al3)

_____
_____
_____

m) Katika sentensi moja onyesha matumizi mawili tofauti ya kibainishi. (al 2)

_____

n) Andika maana ya nahau: Kunja jamvi (al 1)

_____

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa mchoro wa jedwali. (al 4)
Wanafunzi walipojiandaa vilivyo walifuzu mtihani wao.

4. **ISIMU JAMII**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Nini?Umetumana?
Utatumia chai ya kahawa au majani?
Nataka kachai na katosti!

Tosti ni kumi. Tea is twenty shillings
Mbona unaniletea maji ukisema ni chai?
Samahani customer, ngoja nikuletee moto.

a) Lugha iliyo katika kifungu hiki hutumika katika muktadha upi? (al 1)

_____

b) Eleza sifa nne za matumizi ya lugha katika muktadha huu. (al 4)

_____
_____
_____
_____

c) Toa sababu mbili zinazoonyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (al 2)

_____
_____

d) Orodhesha hatua tatu zinazoweza kuchukuliwa kusuluhisha matatizo yanayokumba Kiswahili nchini Kenya. (al 3)

MTIHANI WA PEAK
MUHULA WA TATU - JANUARI
KIDATO CHA NNE – KISWAHILI KARATASI YA 3

JINA _____ **NAMBARI**_____

SAHIHI _____TAREHE_____

DARASA_____

102/3
KISWAHILI FASIHI
MUDA SAA $2^1/_2$

MAAGIZO KWA MTAHINIWA

a. Jibu maswali manne pekee
b. Swali la kwanza ni lazima
c. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki.
d. Usijibu maswali mawili kutoka shemu moja.

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	1	2	3	4	5	6	7	8	JUMLA

SEHEMU A: HADITHI FUPI

MTIHANI WA MAISHA NA EUNICE KIMALIRO

1. LAZIMA

"Pesa aliyonipa baba tuseme imekwenda bure? Imekwenda kama chendacho kwa mganga kisichokuwa na marejeo?

a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (al 4)

b) Taja mbinu **nne** za lugha zilizotumika katika dondoo hili (al 4)

c) Fafanua sifa zozote **nne** za mzungumzaji (al 4)

d) Kwa kurejelea hadithi 'mtihani wa maisha' tathmini changamoto zozote zinazokumba

sekta ya elimu. (al 8)

SEHEMU YA B

RIWAYA: CHOZI LA HERI: ASSUMPTA MATEI (al 20)

2. Eleza jinsi **maudhui ya ufisadi** yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya **Chozi la Heri.** (al 20)

AU

3. *"…….liandikwalo ndilo liwalo? since when has man ever changed his destiny?"*

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)

b) Bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (al 6)

c) Kwa kuzingatia hoja **kumi**, jadili jinsi ambavyo hali ya, **liandikwalo ndilo liwalo",** inavyojitokeza katika Chozi la Heri. (al 10)

SEHEMU C

TAMTHILIA: KIGOGO

4. "Huo ni mradi mzuri, umefadhiliwa kutoka nje."

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (al 4)

b) Eleza sifa **mbili** za msemaji (al 2)

c) Kwa kurejelea dondoo hili na tamthilia kwa jumla, faafanua jinsi mwandishi amefanikiwa katika matumizi ya mbinu ya kinaya. (al 14)

AU

5. Tamthilia ya Kigogo haijapitwa na wakati. Thibitisha ukweli wa kauli hii. (al 20)

6. SEHEMU YA D: USHAIRI

Jibu swali la sita au la saba

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

Msambe naja kuteta, nina wema wa kalima,
Moto wanikatakata, maini yangu yachoma,
Ili nipate takata, ukweli wote 'tasema,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Bahati ni kama nyota, humemeta na
Kuzima, Sikimbilie mafuta, ukatae
Kula sima, Anayekataa pema, pabaya
Panamuita.

Haraka zina matata, angaza mbele na
Nyuma, Tenda mambo kwa kusita,
Usije ukalalama, Keti pako ukipata,
Kwa muradi wa uzima, Anayekataa
Pema, pabaya panamuita.

Pema si penye mafuta, au pa wali
Na nyama, Pema watu hutafuta,
Utulivu na hekima, Si hoja penye
Ukata, pa watu hali ya nyuma,
Anayekataa pema, pabaya
Panamuita

Mahali pema ambata, kwa vitendo na huduma,
Sikae penye matata, palipojaa hasma,
Lau kama pamemeta, hapafai kwa daima,
Anayekataa pema, pabaya panamuita

Maswali

a) Lipe anwani mwafaka shairi hili. (alama 1)

b) Bainisha bahari mbili za shairi hili. (alama 2)

c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

d) Fafanua dhamira ya mshairi. (alam 1)

e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

f) Onyesha jinsi mshairi alivyotumia uhuru wake. (alama 3)

g) Kwa kutoa mifano, bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)

h) Eleza maana ya msamiati ufuatao. (alama 3)

i) Kalima
ii) Mafuta
iii) Ukata

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Mbiu naipuliza, kwawa hapana ng'ambo,
   Kwa aningoja 'mesikia, inaumiza matumbo,
   Kwa upole sitafyoa, hata kamna kwa kimombo,
   Yafaa jihadharia, maisha ya s'ende kombo.

2. Maisha ya s'ende kombo, kututoa yetu ari,

Zingatia haya mambo, wetu wale zimukiri,
Kuwa wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri
watunzeni na maumbo, msie zusha hatari.

3. Msije zusha hatari, na nyingi hizi zahama,
   Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama
   Twaelezea kwa uzuri, matendoyo yatuuma
   Watoto tunayo mori, ni lini mtaja koma?

4. Ni lini mtaja koma, na pombe siso halali?
   Sio baba sio mama, mbona ny' hamtajali?
   Mwafa ja nzi twasema, mwatua chabi la hali
   Hangaiko acha nyuma, kwani hamuoni hili?

5. Kwani hamuoni hili, kila saa mwapigana
   Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona
   Mwatusumbua akili, twaumia ten asana
   Achene na ukatili, kwani upendo hamna.

6. Kwani upendo hamna, kamam mbwa mwatuchapa
   Mwatuchoma sisi wana, mio yetu yatupapa
   Pa kujificha hatuna, tumebaki tukitapa

7. Tumevujwa na mifupa, hata leo uke wetu,
   Mwatubaka na kuapa, kutung'ata nyi' majitu,
   Hayo makeke na pupa, mtakoma utukufu

8. Mtakoma utukufu, nakutumia miki
   Na tabia zenye kutu, tumechoka nayo chuki
   Hatutakubali katu, kutendewa yenye siki
   Serikali fanya kitu, kwani nasi tuna haki

Maswali

a) Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

b) Taja nafsi nne katika shairi hili. (alama 1)

c) Eleza bahari mbili zinaowakilishwa katika shairi hili. (alama 4)

d) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)

e) Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)

f) Eleza umuhimu wa mbinu mbili amabazo mshairi ammetumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. Katika jamii ya Iteso watoto pacha huchukuliwa kama mkosi. Kwa hivyo, hubidi sherehe maalum ifanywe ili kutakasa wazazi wa watoto hawa. Sherehe hii hufanyika siku tatu baada ya kuzaliwa kwa watoto mapacha.

(a) Tambua kipera kinachodokezwa na maelezo haya na ukifafanue (al 2)

(b) Fafanua umuhimu wa kipera cha fasihi ulichotambua katika (a) (al 8)

(c) Fafanua sifa zozote tano za soga. (al 5)

(d) Ni changamoto zipi zinazoweza kumkumba mtafiti akifanya utafiti wa soga nyanjani. (al 5)

SHULE YA UPILI YA MANGU

JINA: _____

NAMBARI YA USAJILI _____ TAREHE _____

KAR 102/1

INSHA

KIDATO CHA NNE

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU /

MUDA: SAA 1 ¾

MAAGIZO:

 KWA MAJIBU PIGA SIMU AMA UTUME UJUMBE KWA BWANA CHEPKWONY 0724351706

- ✓ Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima
- ✓ Kisha chagua insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.
- ✓ Insha yako isipungue maneno 400
- ✓ Kila insha ina alama 20.

1.Wewe ni Mkurugenzi wa tume ya kupambana na ufisadi nchini. Andika barua pepe kwa watumishi wote wa umma ukiwaeleza athari za ufisadi kwa taifa.

2.Teknolojia ya kisasa ina athari mbaya katika maisha ya vijana. Jadili.

3.Andika insha itakayodhirisha maana ya methali ifuatayo: Mzaha mzaha hutumbuka usaha.

4. Andika kisa kitakachomalizika kwa … hivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha Yangu ulivyofunguka.

SHULE YA UPILI YA MANGU

JINA: _____

NAMBARI YA USAJILI _____ TAREHE _____

102/2

KISWAHILI – KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO

a)Andika jina yako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

b)Tia sahihi yako kasha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.

c)Jibu maswali yote.

d)Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

e)Majibu yote lazima yaandikwe kwa Kiswahili.

f)Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA

1		
2		
3		
4		
JUMLA	**80**	

1.UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti na yale ya wanawake waliosihi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamake –kuu.

Yeye hatarajii kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia watoto, na daima dawamu kuwa **"mwandani wa jikoni"** akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani, kuchanja kuni,, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. **Akanyagapo mume naye papo huutia wayo wake.**

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo yake ya lugha, historia, jiografia, hesabu, sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega, akazifanya. Akitaka kuwa mwalimu, akawa. Akataka kuwa daktari, akafanikiwa. Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi wahandishi, madereva wa magari, mawakili, mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wananchi. Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa **hateswi akafyata ulimi**. Anapohiniwa yeye hupigania haki kwa dhati na hamasa. Katu hakubali'mahali pake' katika jamii alipotengwa na wanaume wenye mawazo ya kihaidhina yaliyopitwa na wakati.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake, iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha **ukutani**.

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanaume wa 'kisasa', ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani yale ya akale, lakini wapi! Analazimika kukubali mwanamke huyu kama mshirika sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya **aushi**.

MASWALI

a)Msemo '**mwendani wa vijungu jiko'** unadhihirisha hali gani ya mwanamke katika jamii? (al.2)

b)Jamii imefanya mwanamke kuwa hayawani wa mizigo. Fafanua. (al.2)

c)Eleza maana ya **'akanyagapo mume papo huutia wayo wake'** (al.2)

d)Mlinganishe mwanamke wa kiasili na wa kisasa katika maswala ya ndoa na elimu. (al.4

e)Mwanamume wa kisasa anamwonaje mwanamke wa kisasa? (al.2)

f)Eleza maana ya:

(i)Akafyata ulimi (al.1)

……

(ii)Ukatani (al.1)

……

(iii)Taasubi za kiume (al.1)

…….

2.MUHTASARI / UFUPISHO

Soma kifungu kisha ujibu maswali.

Imesemekana na kurudiwa tena na tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umaskini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya Wakenya milioni kumi wamo katika hatari ya kufa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuatia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo.Imesahaulika kuwa karibu asilimia sabini na tano ya Wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa wananchi na pia kuletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mauzo ya mazao katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa maswala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linatokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja.

Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia sabini na tano ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idadi hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo.Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo haya umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya uchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia ili kumaliza njaa na umaskini. Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kuhusu mihimili ya zaharaa kama vile uzalishaji wa matunda na

mboga, ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kufadhili kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo. Bila hilo hatutakuwa na linguine bali kukimbilia mataifa yalistawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu na njaa.

a)Fupisha aya mbili za mwanzo (maneno 50 – 55) (al.6, 1 ½ ya mtiririko)

(b)Bila kubadili maana,fupisha aya mbili za mwisho. (maneno 55 – 60) (al.6, 1 ½ utiririko)

Matayarisho

……

3.MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a)Taja sauti zenye sifa zifuatazo. (al.2)

i)Irabu ya mbele, juu, tandazwa.

……

ii)Kiyeyusho cha midomo.

……

b)Tofautisha kati ya silabi funge na silabi wazi na utolee mifano. (al.2)

……

……

……

……

c)Eleza dhima ya sentensi ifuatayo. (al.1)

Naomba uniazime kalamu yako.

……

……

d)(i)Eleza maana ya mofimu. (al.1)

……

……

……

(ii)Ainisha mofimu katika neon

alani? (al.2)

……

e)Tambua aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo: (al.3)

Hawa sio walimu bali wamekuwa wakifunza katika shule hii.

……

……..

……..

……..

f)Weka neno hili katika ngeli mbili tofauti : (al.2)

Maziwa

……..

g)Eleza tofauti iliyopo kati ya ukanushaji na kinyume. (al.2)Andika kinyume cha

Kibe alikunja nguo zilizoangikwa ukutani alama 1

……

Kanusha

Kibe alikunja nguo zilizoangikwa ukutani alama 1

……..

h)Andika katika wingi: (al.2)

Zigo la kuliwa halilemei.

……

……

i)Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo wingi. (al.2)

Meza ilianguka ikavunjika tendeguu.

……

)Tunga sentensi mojamoja ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa mabanoni. (al.2)

Paka (tendata)

……

Choma (tendua)

……

k)Tumia nomino mji kama kielezi cha mfanano. (al.1)

……

……

l)Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno walakini na uzitaje. (al.2)

……

……

……

……

m)(i)Tunga moja sentensi ambatano.(al.2)

……

……

(ii)Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi . (al.4)

Mbwa pamoja na paka walikuwa wakiuzwa sokoni.

n)Ainisha virai katika sentensi ifuatayo:

Wote wanne walijificha nyumba ya mlango.

……

……

……

o)Onyesha aina za vishazi katika sentensi ifuatayo. (al.2)

Babake alipofika nyumbani alipumzika kitandani.

……

……

……

p)Andika sentensi **moja** yenye shamirisho zifuatazo. (al.3)

kipozi, kitondo na ala.

……

……

q)Andika sentensi ifuatayo katika msemo wa taarifa.

"Tutawapa zawadi zenu kesho mkija na wazazi," mwalimu aliwaambia.

……

……

……

r)Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia kisawe cha neno lililopigiwa mstari. (al.1)

Babangu hapendi kunywa pombe.

……

……

s)Tofautisha sentensi. (al.2)

(i)Ungalisoma kwa bidii, ungalipita mtihani.

……

……

ii)Ungelisoma kwa bidii, ungelipita mtihani.

……

……

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

"Naona 'Horse Power' mwenyewe ndiye atakayepiga,….. atakayecheza foul hiyo. Wachezaji wa ……."

a)Tambua sajili inayorejelewa. (al.2)

……

……

……

b)Tambua sifa zinazobainisha sajili yenyewe. (al.8)

……

……

……

……

……

……

……

……

SHULE YA UPILI YA MANGU

JINA: _____

NAMBARI YA USAJILI _____ TAREHE _____

102/3

KISWAHILI FASIHI

KARATASI YA 3

MUHULA WA PILI

MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO

a)Jibu maswali manne pekee.

b)Swali la kwanza ni la lazima.

c)Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani Tamthiliya fupi, Ushairi na Riwaya.

d)Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

e)Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
	20	
	20	
JUMLA	**80**	

SWAli 1 LAZIMA SEHEMU YA : FASIHI SIMULIZI

Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu. Wanyama hawa waliishi baharini.Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba.Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika.Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa.Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza . Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka. Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

MASWALI

a)Tambua utanzu na kijipera chake. (al.2)

b)Taja fomyula zingine **mbili** za kutanguliza kifungu hiki. (al.2)

c)Eleza umuhimu wa kijipera hiki. (al.5)

d)Eleza sifa za kifungu hiki. (al.5)

e)Eleza umuhimu wa fomyula:

(i)Kutanguliza (al.3)

(ii)Kuhitimisha (al.3)

SEHEMU YA B : TAMTHILIA (P.KEA KIGOGO)

Jibu Swali la pili au la tatu.

2 "…… Udongo haubishani na Mfinyanzi. Acha porojo zako. Kigogo hachezewi; watafuta maangamizi!"

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b)Fafanua mbinu **mbili** za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. (al.2)

c)Eleza sifa zozote **nne** za msemaji. (al.4)

d)Onyesha ukweli wa kauli hii katika dondoo hili ukirejelea hoja **kumi**. (al.10)

AU

3.a)Tatizo la uongozi katika bora la Afrika ni kikwazo kikubwa cha maendeleo. Kwa kurejelea matukio kwenye Tamthilia ya Kigogo. Jadili ukweli wa kauli hii. (al.10)

b)Eleza mbinu alizotumia Majoka kufanikisha utawala wake. (al.10)

SEHEMU YA C : RIWAYA (A.MATEI : CHOZI LA HERI)

Jibu swali la nne au la tano

4."Lakini itakuwaje historical injustice, nawe Ridhaa hapo ulipo sicho kitovu chako?"

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b)Eleza tamathali **mbili** za lugha zilizotumika kwenye dondoo hili. (al.4)

c)Fafanua sifa **tatu** na umuhimu tatu wa msemaji wa maneno haya. (al.6)

d)Taja mambo **sita** yaliyowakumba wale ambao kitovu chao sicho walicho? (al.6)

AU

5.a)"Siasa mbaya maisha mabaya."Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri. (al.10).

b)Fafanua athari za umaskini katika jamii ukirejelea Riwaya ya Chozi la Heri.

SEHEMU YA D : HADITHI FUPI (Alifa Chokocho na D.Kayanda (Wahariri)

Jibu swali la sita au la saba.

6."Lazima niache kazi maana mume wangu haniamini."

a)Fafanua muktadha wa dondoo hii. (al.4)

b)Eleza sifa **sita** za mzungumzaji katika dondoo hili. (al.6)

c)Eleza mbinu zifuatazo kama zilivyotumika katika hadithi.

(i)Sadfa (al.6)

(ii)Majazi (al.4)

AU

7.”Hatuwezi kumaliza kula, kila leo tuna kula”.

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b)Fafanua tamathali ya usemi iliyotumika. (al.2)

c)Eleza umuhimu wa mnenaji. (al.4)

d)”Lakini nakwambia tena, kula kunatumaliza”. Kwa kudokeza hoja **kumi** jadili ukweli wa kauli hii. (al.10)

SEHEMU YA E : USHAIRI

HEKO JESHI LETU

Hebu niwatangazieni, mitimani yalotanda,

Katu si ya furahani, bali ya mori kupanda,

Kenya yetu I motoni, Al Shabaab katenda,

Katuchokoza yakini, kututeka kama punda,

Lo! Vyombo vya baharini, kwa telki kavidanda.

Wakashambuliya pwani, watalii wakadinda,

Kawapora mifukoni, ilo ndarama mabunda,

Maguruneti jijini, mabomu ja parapanda,

Waasi hawa kidini, kajifunga kwa magwanda,

Wakavuruga amani, ya wakenya waso inda.

Hawa sisi twalaani, kwa usalama kuvunda,

Toka Somalia baini, kuteka Kenya kapenda,

Ndo kavamiya wageni, kisha nao wakaenda,

Kawatesa matekani, kuwafunga kwa mikanda,

Sote kajawa huzuni, kutendewa kama kinda.

Wanajeshi wa nchini, chonjo pasi kusarenda,

Wakenda hivyo vitani, nyoyo bila kuwatunda,

Ka'nzisha operesheni, ya jeshi nchi kulinda

Kajitoma mipakani, huku vikosi meunda,

Somalia sadikini, kawa wa kondo ukanda.

Kwa silaha mikononi, mahandakiyo karanda,

Vita vya anga, jangwani, kulo maji na migunda,

A'Shabab nuksani, kamegwa mfano tunda,

Chao kawa hatarini, wanajeshi kawawinda,

Mchana piya jioni, ngomezi zao kaganda.

Wanamgambo sikieni, kazingirwa kikandanda,

Kavunjavunjwa usoni, miguuni piya vyanda,

Kahasiriwa mwilini, huku kabaki mepinda,

Haramia kawa duni, wakangamizwe manunda

Jeshi kajitahidini, matunda mema katunda.

Habari ulimwenguni, kamoma propaganda,

Kuenezeka kampeni, nazo nchi kama Rwanda,

Jeshi kajitoleeni, siku kadha' za kalenda,

Jeshi letu shukurani, kutulinda ja makinda,

Twakusihi E Manani, tujali kwa kutupenda.

MASWALI

a)Pendekeza kichwa kingine kinachofaa shairi hili. (al.1)
b)Onyesha toni ya shairi hili. (al.1)
c)Eleza nafsi neni katika shairi hili (alama 1)
c)Ni madhila gani yametendwa na Al Shabab? (al.6)
d)Fafanua uhuru wa kishairi uliotumiwa na mtunzi katika ubeti wa pili. (al.4)
e)Eleza muundo wa shairi hili. (al.4)
f)Eleza maana ya maneno haya yalivyotumwa na msanii. (al.3)
i)Magwanda.
ii)Mahandaki

iii)Maharamia

102/1
KISWAHILI
Karatasi 1
Muda: Saa 1¾

KENYA HIGH EXAMINTIONS

Andika insha MBILI. Insha ya KWANZA ni ya LAZIMA.
Chagua insha moja nyingine kutoka tatu zilizobaki.
Kila Insha isipungue maneno 400.
Kila Insha ina alama 20.

INSHA 102/1

1. **Lazima :**

Wewe ni mwenyekiti wa jopo lililoteuliwa kuchunguza chanzo cha utovu wa usalama kijijini Sokoto. Andika ripoti maalum /rasmi kuhusu jambo hili.

2. Magonjwa mengi yanasababishwa na mitindo ya kisasa ya maisha.
   Jadili.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mchagua nazi hupata koroma.

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno haya:

Milipuko mikubwa ilisikika pu! Pu! Puu! Kisha niliwaona watu wakikimbia kuelekea

pande zote…

Jina……Nambari yako……/……

Tarehe ….……..Sahihi yako…….……

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

MUDA: SAA 2 ½

KENYA HIGH EXAMINTIONS

KIDATO CHA NNE

MAAGIZO

1. Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulioachiwa hapo juu.
2. Weka **sahihi yako** na **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
3. Jibu maswali yote.
4. Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali.

Kwa matumizi ya mtihani pekee.

swali	**upeo**	**alama**
1 2 3 4	15 15 40 10	
Jumla	80	

Karatasi hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1. **UFAHAMU: (Alama 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanaoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hili husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto, awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hili walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. Inakera zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa Jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea had kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa, ni kweli. Hata hivyo, wengi hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21, asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyishwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo nakuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa

ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata awaoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale hushia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine hushia kutumiwa kama watumwa wa 'kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali 'mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

Maswali

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 1)**

_____

_____

b) Eleza dhana ya mwanamkiwa kwa mujibu wa kifungu. **(alama 2)**

_____

_____

_____

_____

c) Eleza imani za kijadi kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 2)**

_____

_____

_____

_____

d) Jadili masaibu yanayowakumba wanawakiwa. **(alama 4)**

_____

_____

_____

_____

_____

e) Eleza haki mbili za kikatiba zilizokiukwa kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 4)**

_____

_____

_____

_____

_____

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu. **(alama 2)**

i) Inakera

_____

_____

ii) Majukumu

_____

_____

2. **UFUPISHO: (Alama 15)**

<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali</u>

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundishia. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkemu kwa mtu wa kila rika. Halikadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji wa stadi ya kujifundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemchemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanaowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii. Ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala

yake, tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaotumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

a) Fupisha aya tatu za kwanza za (maneno 70 – 75) (alama 7, 2 za utiririko)

Matayarisho

_____

b) Eleza udhaifu wa runinga na video. (maneno 50 – 51) (alama 5, 1 ya utiririko)

Matayarisho

MATUMIZI YA LUGHA: (alama 40)

a) Taja aina mbili kuu za ala za kutamkia sauti **(alama 2)**

_____

_____

_____

b) Taja mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo **(alama 2)**

Kimadende_____

Kipasuo kwamizo_____

c) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi sahili **(alama 2)**

_____

_____

_____

_____

d) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo **(alama 3)**

Tulimpikia_____

e) Ainisha vitenzi katika sentensi: Kitabu anachotaka kusoma ki mezani **(alama 3)**

_____

_____

_____

_____

_____

_____

f) Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi kiteuzi **(alama 2)**

_____

_____

_____

g) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama 2)**

a) Uzi_____

b) Muda_____

h) Tumia ‘o’ rejeshi ya kati katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Watu ambao walifika jana ni wale ambao walitoka mbali

_____

i) Onyesha shamirisho kipozi na ala katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mwindaji haramu alimuua ndovu kwa bunduki

_____

_____

_____

j) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 3)**

Kilipikwa jana jioni

_____

_____

_____

k) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi **(alama 2)**

Msingesoma kwa bidii, msingepita

l) Tunga sentensi moja kudhihirisha dhamira/jukumu hili **(alama 2)**

Rai/ombi

m) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mtoto ambaye alianguka jana ana maumivu mengi

n) Onyesha matumizi yoyote mawili ya kiwakifishi: koma/kituo **(alama 2)**

o) Tumia neno 'Nairobi' kama **(alama 2)**

a) Nomino

b) Kielezi

p) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya kuku na gugu **(alama 2)**

_____

_____

q) Onyesha matumizi ya kiambishi -ji- katika sentensi **(alama 2)**

Mwongeleaji stadi anajishaua sana.

_____

_____

_____

r) Andika katika usemi wa taarifa **(alama 2)**

"Wageni wangu watafika saa ngapi? Mama aliuliza

_____

s) Unda nomino kutokana na kitenzi **(alama 1)**

Safari

_____

ISIMUJAMII: **(alama 10)**

Nipe chai, andazi mbili na egg moja…….

a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya **(alama 2)**

b) Fafanua sifa nne zinazohusishwa na sajili hiyo **(alama 8)**

KENYA HIGH EXAMINTIONS

MTIHANI WA MWIGA – MWIGO

Jina_____

Nambari_____

Sahihi ya mtahiniwa_____

Tarehe_____

KISWAHILI
KARATASI YA 3, FASIHI 1, MUHULA WA PILI
MUDA: 2 ½
MAAGIZO

(a) Jibu maswali manne pekee.
(b) Swali la kwanza ni lazima.

(c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliww kutoka sehemu nne zilizobaki
(d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

SEHEMU A: Riwaya

1. LAZIMA

Assumpta K. Matei: Chozi la heri

"Hili lilimtia ……. uchungu, akajiona kama aliyedhalilishwa na mwanamke."

(a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake (alama 4)

(b) Taja suala linalodokezwa katika dondoo hili (alama 1)

(c) Kwa kutumia hoja kumi na tano, eleza namna suala ulilolitaja hapo juu 1 (b) linalijitokeza (ala. 15)

SEHEMU B: Tamthilia

Kigogo (Pauline Kea)

Jibu swali la pili au la tatu

2. "Kubali pendekezo letu la kufungwa kwa soko…… huoni hii ni fursa nzuri ya kulipiza kisasi?"

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Kufungwa kwa soko ni ukatili. Mbali na ukatili huu, toa mifano mingine ya ukatili kwenye tamthilia. (alama 9)

(c) Msemaji wa maneno haya ni mshauri mbaya. Thibitisha kutoka kwenye dondoo na kwingineko tamthiliani. (alama 7)

3. (a) Fafanua mbinu kumi anazotumia Majoka katika kuuendeleza uongozi wake(alama 10)

(a) Eleza namna mbinu ya ishara ilivyotumiwa katika tamthilia ya Kigogo (alama 10)

SEHEMU C: Hadithi Fupi

Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine (Alifa Chokocho na Dumu Kayanda)

Jibu swali la 4 au la 5

4. "…… Ningeondoka ….. mapema niende niibe au niue ili niwe mtu wa maana."

(a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)

(b) Onyesha vile Kinaya kinavyojitokeza katika dondoo hili (alama 2)

(c) "Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi husika. Thibitisha kwa kutumia hoja tisa (alama 9)

(d) Eleza umuhimu wa msemaji katika hadithi hii (alama 5)

5. (a) Eleza namna maudhui ya ndoa yalivyosawiriwa katika hadithi ya Masharti ya Kisasa (alama 13)

Kwa kurejelea hadithi ya Shibe inatumaliza, eleza namna maudhui ya ufisadi yanavyojitokeza (alama 7)

SEHEMU D: Fasihi Simulizi

6. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali

Heri ujue mapema
Nasaba yetu haina woga
Woga haumei kwetu, humea kwa kina mamako.
Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume.

Ah! Kisu cha ngariba ni kikali ajabu.
Iwapo utatikisa kichwacho.
Uhamie kwa wasiotahiri,

Ama tukwite njeku.

Mpwangu kumbuka hili,
Wanaume wa mlango wetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku
Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa
Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope
Wasichana wa kwetu na wa mbali
Wote watakucheka
Ubaki ukinuna.

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia
Sema unachotaka
Usije kunitia aibu

Maswali;

(a) Taja na uthibitishe shughuli zozote za kiuchumi za jamii ya wimbo huu (alama 4)
(b) Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anawaimbia nani? (alama 2)
(c) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha (alama 2)
(d) Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume. Thibitisha kauli hii. (alama 2)
(e) Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii (alama 6)
(f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii (alama 4)

SEHEMU E: Ushairi (alama 20)
Jibu swali la 7 au la 8

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Kama dau baharini, duniya inavyoyumba,
Limeshamiri tufani, kila mmoja lakumba,
Viumbe tu hali gani!

Duniya yatishika, utahisi kama kwamba,
Vilima vyaporomoka, na kuvurugika myamba,
Viumbe tu hali gani!

Tufani hilo la kusi, languruma na *kutamba*,
Linapuliza kwa kasi, hapana kisichoyumba,
Viumbe tu hali gani!

Mujiwe ni kubwa sana, mfanowe kama nyumba,

Yazuka na kugongana, wala hatuna la *kwamba*,
Viumbe tu hali gani!

Mibuyu hata mivule, kama usufi na pamba,
Inarusha vilevile, *seuze hiyi migomba*
Viumbe tu hali gani!

Ni kipi kilotuliya, tuwazeni na kudumba,
Mandovu kiangaliya, yagongana na masimba,
Fisi wako hali gani!

Hata papa baharini, tufani limewakumba,
Walioko mikondoni, kila mmoja *asamba*,
Dagaa wa hali gani!

Mashehe wa mdaduwa, kwa ubani na uvumba,
Tufani hilo kwa kuwa, kusoze kwake kutamba,
Itokee afueni!
(Shairi la 'Tufani' la Haji Gora Haji, katika *Tamthilia ya Maisha*, uk 62)

Maswali;

(a) Taja na ueleze mikondo ya shairi hili (alama 4)
(b) Eleza dhamira ya shairi hili (alama 2)
(c) Taja tamathali za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
(d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)
(e) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano. (alama 3)
(f) Onyesha matumizi ya idhini ya kishairi . (alama 3)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mjibu wa shairi hili (alama 2)

(a) Mdaduwa :
    (a) Kutamba :

8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Daima alfajiri na mapema

Hunipitia na jembe na kotama

Katika njia iendayo Kondeni

Kama walivyofanya babuze zamani;

Nimuonapo huwa anatabasamu

Kama mtu aliye na hamu

Kushika mpini na kutokwa jasho

Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza

Videge vya anga vinavyotumbuiza

Utadhani huwa vimemngojea

Kwa usiku kucha kuja kumwimbia
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimtetea
Nao umande kumbusu miguuni;

Na miti yote hujipinda migogo
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kundelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akichekelea ha ha ha ha ha ha …….

Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani?
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho.
Kuna jambo gani linalomridhisha?
Kama si kujua ni kutojua
Lait angalijua, laity angalijua!

Maswali:

a) Eleza hali ya mzungumziwa katika shairi hili. (alama 2)
b) Huku ukitoa mifano, onyesha aina mbili za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili (ala. 4)
c) Fafanua aina tatu za taswira ukirejelea ubeti wa pili (alama 3)
d) Maswali ya balagha katika shairi hili yanasisitiza maudhui yapi? (alama 2)
e) Kwa kutoa mifano, bainisha vipengele vitatu vya Kimtindo katika shairi hili (alama 3)
f) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)
g) Bainisha nafsineni katika shairi hili (alama 1)
h) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)

Jina…….....Nambari……../……...

Shule…….Sahihi……..

Tarehe…….

102/3 (*Fasihi*)

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FEB

Muda: Saa 2 ½

SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA MOI NAIROBI

Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari- Kenya (KCSE)

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Saa 2 ½

MAAGIZO KWA MTAHINIWA

a) *Jibu maswali manne pekee*

b) *Swali la kwanza ni la lazima*

c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani : riwaya, Tamthlia, hadithi fupi, ushairi na fasihi simulizi.*

d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	1	2	3	4	5	6	7	8	Jumla

 KWA MAJIBU PIGA SIMU AMA UTUME UJUMBE KWA BWANA CHEPKWONY 0724351706

SEHEMU YA A.

SWALI LA LAZIMA. (FASIHI SIMULIZI)

1. (a) i) Eleza sifa **sita** za maghani. (alama 6)

(ii) Fafanua dhana zifuatazo (alama4)

a) Rara
b) Tondozi
c) Sifo
d) Pembezi

(b) Tofautisha kati ya malumbano ya utani na maapizo. (alama 2)

(c) Fafanua sifa nne za malumbano ya utani (alama 4)

(d) Jamii ya kileo inaendelezaje fasihi simulizi? (alama 4)

SEHEMU YA B. RIWAYA: CHOZI LA KHERI (Assumpta K. Matei.)

(Jibu swali la 2 au la 3)

(2) "Nitapigana kwa jino na ukucha kuulinda utu wangu."

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b. Eleza umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (alama 4)
c. Kwa kutolea mifano riwayani, thibitisha namna binadamu alivyopungukiwa na utu. (alama 12)

(3) Mwanamke ametwezwa katika kiwango sawa na namna alivyotukuzwa. Thibitisha ukweli wa madai haya kwa kurejelea riwaya ya *Chozi la Heri.* (alama 20)

SEHEMU YA C. TAMTHILIA : KIGOGO (Pauline kea)

(Jibu swali la 4 au la 5)

(4) Mhusika A:Watu wa(Sagamoyo mu wajinga sana.
Mhusika B:Mzee,Stop it.....stop it please.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Taja na ueleze mbinu ya lugha iliyotumiwa katika muktadha huo (alama 2)
c) "Watu wa Sagamoyo" wana umuhimu gani katika mutadha huu. (alama 6)

d) Jadili maana na matumizi ya JAZANDA ZIFUATAZO kama zilivyotumiwa katika Tamthilia. (alama 8)

i. Mdomo wa simba
ii. Keki
iii. Panya amejileta kwa paka
iv. Mshumaa haupotezi mwangaza kwa kuwasha mshumaa mwingine.

(5) "udongo haubishani na mfinyanzi"

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

(b) Thibitisha kwa kutoa **mifano kumi** kuonyesha ukweli wa kauli kuwa udongo haubishani na mfinyanzi. (alama 10)

(C) "Hawakuvunja mguu wa kitamathali…"

i. Taja na ueleze sifa **tatu** za anayelengwa katika tamko hili. (alama 3)
ii. Eleza umuhimu wa anayerejelewa katika tamko hili. (alama 3)

SEHEMU YA D. HADITHI FUPI

TUMBO LISILOSHIBA na hadithi nyingine (wahariri: A. Chokocho na D. Kayanda)

(Jibu swali la 6 au la 7)

(6) Kidege

"Ingawa vingi , sauti havina sauti zavyo zinamezwa tu na mipumuo……."

(a) Eleza muktadha huu (alama 4)

(b) Onyesha namna maudhui ya ukatili yanajitokeza katika hadithi hii. (alama 16)

(7) Shibe inatumaliza; Salma Omar

(a) Jazanda ni mojawapo ya mbinu za lugha zilizotumiwa kwa ukamilifu. Ukirejelea hadithi shibe inatumaliza fafanua mifano kumi. (alama 10)

Mame Bakari Mohammed Khelef

(b) Athari za ubakaji ni donda sugu katika jamii. Thibitisha kauli hii kwa mujibu wa hadithi hii. (alama 10)

SEHEMU YA E: USHAIRI

(Jibu swali la 8 au la 9)

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata

(8) Uliza wanaojua

Wako wapi waliokuwa viongozi zamani
Waliokitoa hotuba ujamaa kuupigania?
Sasa wamestaafu ndio wafuga kuku
Ndio wenye majumba ubepari kurithisha!
Kama wewe hujui, uliza wanaojua
Ukweli watakwambia.

Au hujaona makabaila wenye mashamba.
Matrekta yanafukuta na vumbi kutimuliwa!
Zungumza juu ya vijiji watakuonyesha kidole
"Pilipili usiyoila yakuwashiani!"
Basi, kama wewe hujui, uliza wanaojua
Ukweli watakwambia.

Lakini Darubini la Serikali ni kubwa sana
Tena lina nguvu sana na lina sumaku.
Linawavuta wakapimwa
Chote walichokwisha kula kikaonekana.
Rafiki, kama wewe hujui, basi uliza
Wanaojua. Ukweli watakwambia.

Hata dawa ya kutapisha Serikali inayo
Mabepari na Makabaila wametapishwa hadharani
Wakaona na aibu mbele ya wake zao.
Wananchi tuliwazomea tena tukacheka sana.
Ndugu, kama wewe hujui, basi usinyamaze.
Uliza wanaojua. Ukweli watakwambia.

Maswali:

(a) Thibitisha kwamba hili ni shairi. (alama 3)

(b) Jadili matumizi ya kinaya katika shairi hili. (alama 4)

(c) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alama 4)

(d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

(e) Eleza matumizi yoyote mawili ya mishata. (alama 2)

(f) Bainisha nafsi-nenwa katika shairi hili. (alama 1)

(g) Thibitisha kuwa mabadiliko hayaishi duniani kwa kurejelea shairi hili. (alama 4)

(9) Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata

Ndege mwema na muruwa, katu haishi tunduni
Hataki kufadhiliwa, muda yumo utumwani
Japo mnyonyoe mbawa mwisho wake atahuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa.

Ndege ataka yoyoma, nasiyahi msituni
Apite akisimama, shinani na mitawini
Haridhiki kwa mtama, na maji ya kikombeni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa hishima mwema mno wa kughani
Tundu huliona chama, japo liwe la thamani
Huporomosha yakwe kima, na kufanya faraghani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mpambe kwa zari, na lulu na marijani
Upambe yake suduri, kwa almasi kidani
Tunduni atahajiri, ili awe huriani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa busara, hatoishi kifungoni
Anayo kubwa hasara, kukosa nyumba ya mani
Lamkera lamkera, tundu la dhahabu kwani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege maumbile yake, na waja hayalingani
Yeye hutaka wenzake wafukuzane hewani
Jambo la kuishi mpweke, kamwe humridhiani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Baiti zangu ni haba, nakonea kituoni
Ndege huficha mahaba, kama yumo kifungoni
Hali ndege akashaba, kwani yumo adhabuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

<u>Maswali</u>

(a) Lipe shairi anwani mwafaka (alama 1)
(b) Fumbua maana ya ndege anayerejelewa (alama 1)
(c) Shairi hii ni la mkondo gani? (alama 3)
(d) Eleza muundo wa ubeti wa nne (alama 3)
(e) Fafanua uhuru aliotumia mshairi (alama 4)
(f) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 4)
(g) Jadili dhamira ya mshairi (alama 2)
(h) Fafanua maana ya msamiati ufuatao kama ilivyotumiwa na mshairi (alama2)
    i) Atahuni
    ii) Baiti

Jina: ..... **Nambari: .....**

Darasa: ..... **Sahihi .....**

Tarehe: …….....……

102/1

KISWAHILI
KARATASI YA 1
MUDA: SAA 1 ¾

MOI HIGH SCHOOL, KABARAK

Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)

KIDATO CHA NNE

MAAGIZO

a) Jibu maswali mawili

b) Swali la kwanza ni la lazima

c) Kisha chagua swali lingine kutoka hayo matatu yaliyosalia

d) Kila insha isipungue maneno 400

e) Kila insha ina alama 20

INSHA

SWALI LA LAZIMA

1. Kama mhariri wa gazeti, andika **tahariri** ukipongeza hatua ya serikali kupiga marufuku matumizi ya karatasi za sandarusi.

CHAGUA MOJA:

2. Eleza njia za kustawisha uchumi uliosambaratika katika eneogatuzi lako.
3. Pwagu hupata pwaguzi.
4. **Andika** insha itakayomalizikia kwa maneno haya.

   "…Nilipokaa mezani kula chakula kitamu, nilikumbuka maisha magumu niliyoyapitia, nikatambua kuwa si rahisi kupata chakula kama hicho bila juhudi maishani"

Jina:……..……..Nambari:……...……

Darasa: …….. Sahihi .....

Tarehe: …….....

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA 2

MUDA: SAA 2 ½

MOI HIGH SCHOOL, KABARAK

KIDATO CHA NNE

MAAGIZO

- *Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- *Weka **sahihi yako** na **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa*
- *Jibu maswali yote.*
- *Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

1. **UFAHAMU:** **(ALAMA 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani. Kunayo saratani ya ngozi – vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopasuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitisha hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung'olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwepesi zaidi ya kawaida. Hii husababishwa na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara

inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kupitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo. Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.

Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika. Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.

Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sahabu uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaoonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano, hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.

Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kinga zake wa kuikinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujikinga dhidi ya vidonda vya tumboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na, ni rahisi kutokea tena baada ya kupona.

Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

Maswali

a) Yape makala haya kichwa. (alama 2)

……

……

……

b) Mbali na athari kwa uzazi kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu. (alama3)

……

……

…….

c) Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara kwa wanawake hasa ni hatari mno. (alama 4)

……

……

……

……

(d) Je, ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu. (alama 2)

……

……

……

……

(e) Eleza namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. (alama 3)

……

……

……

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa. (alama 1)

Gandwa _____

2. **UFUPISHO: (ALAMA 15)**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali:

Biashara ya kimataifa ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ile. Nchi mbalimbali zimekuwa zikitegemeana kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, nchi ya Kenya imekuwa ikiuza maua na mboga katika nchi za ng'ambo na kupata fedha za kigeni ambazo hutumiwa humu nchini kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Biashara ya kimataifa huziwezesha nchi ambazo hazizalishi bidhaa na hata huduma mbalimbali kupata bidhaa hizo kutoka nchi nyingine zinazohusiana nayo katika biashara. Mathalan, Kenya ni nchi ambayo imekuwa ikitegemea kilimo lakini haijaendelea katika sekta ya viwanda. Kenya huagiza bidhaa kama vile vipuri vya magari na hata magari yenyewe kutoka nchi kama vile Japan. Nayo Kenya huuza mazao ya shambani kama vile pareto, chai na kahawa ng'ambo.

Kupitia kwa biashara ya kimataifa, nchi hupata masoko kwa bidhaa zake. Kwa vile biashara ya kimataifa huziwezesha nchi husika kuzalisha bidhaa mahususi ambazo hazitaigharimu nchi pesa nyingi kuzalisha, nchi hizo aghalabu huzalisha kiasi kikubwa cha bidhaa kuliko mahitaji yake ya nyumbani. Nchi basi hulazimika kutafuta masoko nje ya mipaka yake. Kwa njia hii uchumi wa nchi huendelea kuimarika.

Aidha, biashara ya kimataifa huwezesha nchi kupata huduma za kitaaluma ambazo hazipatikini katika nchi husika. Kuna nyanja za kiuchumi ambazo huhitaji wataalamu mahususi.

Kwa mfano, katika sekta ya matibabu nchini humu tumepata kwamba kuna baadhi ya magonjwa ambayo yanahitaji matibabu maalumu. Wanaougua magonjwa haya huagiziwa madaktari kutoka ng'ambo au hata kupelekwa ng'ambo kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

Biashara ya kimataifa hukuza ushirikiano wa kimataifa. Nyakati za majanga ya kimaumbile na hata mengine yanayosababishwa na kutowajibika kwa binadamu, nchi hupata usaidizi kutoka nchi za ng'ambo. Kwa mfano wakati wa mkasa wa bomu wa 1998, Kenya ilipata msaada wa kukabiliana na janga hili kutoka Israeli, Marekani na hata Ujerumani ambako baadhi ya waathiriwa wa mkasa huo walipelekwa kwa matibabu zaidi. Ushirikiano huu wa kimataifa huwezesha wananchi kutoka nchi fulani kwenda kusomea na hata kufanya kazi katika nchi nyingine. Katika miaka ya hivi karibuni Wakenya wengi wamekuwa wakienda kusomea vyuo vikuu vya ng'ambo. Wengine wamediriki kupata kazi katika mashirika ya kimataifa katika nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini, Rwanda, Msumbiji na kadhalika.

Biashara ya kimataifa husaidia kukuza ushindani kati ya nchi husika. Ushindani huu ni hakikisho la uzalishaji wa bidhaa za thamani bora. Kila nchi itafanya juu chini kuzalisha bidhaa ambazo zinaweza kukubalika katika soko la kimataifa. Pia wananchi wa nchi husika hupata aina tofauti za bidhaa badala ya kutegemea aina moja tu ya bidhaa zinazozalishwa nchini mwao.

Biashara ya kimataifa huleta ushirikiano wa kisiasa na uelewano zaidi kati ya madola mbalimbali. Mathalan muungano wa nchi za Afrika Mashariki – Kenya, Uganda na Tanzania, hauchangii tu kuleta manufaa ya kiuchumi bali huleta ushirikiano zaidi wa kisiasa.

Ingawa biashara ya kimataifa ina natija, biashara hii huandamana na hasara mbalimbali. Biashara hii imesababisha kuwapo kwa masoko huru ambayo yameleta ushindani mkubwa kwa wafanyibiashara wadogo wa humu nchini. Baadhi ya wafanyibiashara wamelazimika kufunga biashara zao baada ya kufilisika. Ushuru mkubwa unaotozwa baadhi ya bidhaa nchini huwafanya wananchi wengi kutofaidika kwa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, kuna ucheleweshaji wa bidhaa zilizoagizwa. Bidhaa hizi mara nyingi huchukua muda kabla ya kutoka nchini, kwa hivyo wafanyibiashara wengi hulazimika kungojea kupata bidhaa hizi na kuwauzia wateja wao.

Vilevile, kutokana na biashara ya kimataifa, bidhaa duni huweza kupenyezwa katika mataifa yanayoendelea. Pia baadhi ya wafanyibiashara wa kimataifa huchukua fursa hii kulangua dawa mbalimbali za kulevya ambazo huwaathiri vijana wa nchi husika. Wengine huhusika katika vitendo vya kigaidi kama vile uchomaji wa majengo mbalimbali kwa bomu na mauaji ya ananchi wasio na hatia.

Ni kweli kuwa biashara ya kimataifa ina hasara zake. Hata hivyo mhimili mkubwa wa uchumi wa mataifa machanga.

(a) Kwa maneno yasiyozidi **themanini**, eleza umuhimu wa biashara ya kimataifa.(alama 7)

(b) Kwa maneno yasiyozidi **40**, eleza ujumbe wa aya tatu za mwisho. (alama 6)

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) Sahihisha sentensi: (alama 2)

(i) Mitume hiyo siyo ambayo tunaijua.

……

(ii) Wasikilizaji sasa wanaburudika na muziki kutoka idhaa la taifa hii.

……

(b) Ikanushe sentensi hii katika umoja. (alama 2)

Wasingecheza kiustadi wasingeshinda katika michezo ile.

……

(c) Tambulisha nyakati na hali katika sentensi: (alama 2)

(i) Wachezaji walikuwa wanafanya mazoezi.

…….

……...

(ii) Nkirote alipoingia alitukemea.

…….

……

(d) Eleza maana za sentensi. (alama 2)

(i) Kwa nini wasililie hapa?

…….

……...

(ii) Kwa nini wasilie hapa?

…….

……

(e) Toa mifano miwili miwili ya sauti zinazotamkiwa katika : (alama 2)

(i) ufizi ……

(ii) meno ……

(f) Andika udogo na ukubwa wa neno ‘kidole’. (alama 2)

(i)……(ii)……

(g) Tunga sentensi mbili tofauti kubainisha matumizi ya KWA. (alama 2)

(i)……..……

(ii)……..……...……

(h) Onyesha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Msichana alimkaririra mgeni shairi.

(i) ……

(ii)……

(i) Tumia vitenzi hivi katika sentensi mojamoja katika jinsi ya kufanyiwa. (alama 2)

(i) nywa

……

(ii) pa

……

(j) Kistari kifupi (-) aghalabu hutumika kuendeleza sauti hasa katika vihisishi. Onyesha matumizi mengine matatu ya alama hii akifishi. (alama 3)

(i)…….

(ii)……

(iii)……

(k) Tunga sentensi kubainisha tofauti kimaana kati ya vitawe: (alama 2)

(i)juha……

(ii)jua……

(l) Ziandike upya sentensi hizi kwa mujibu wa maagizo uliyopewa. (alama 2)

(i) Kiyondi aliukomelea mlango alipovisikia vishindo.

(Anza kwa :Mlango……..)

……

……

(ii) Mvua ilinyesha sana alasiri hiyo. Wachezaji walicheza mpira vizuri tu.

(Tumia ‘japo’)

……

……

(m) Tunga sentensi sahihi kubainisha matumizi ya KI kuonyesha: (alama 4)

(i) masharti

……

(ii) ngeli

…….

(iii) kufanyika vitenzi viwili au zaidi wakati mmoja

……

(iv) kielezi namna

…….....

(n)Tambua hali na matumizi ya kisarufi ya neno lililopigwa mstari katika sentensi: (alama 1)

Mtu mzee anapaswa kuheshimiwa

…….

(o) Andika katika usemi halisi. (alama 2)

Mwalimu aliwaagiza wanafunzi warudi darasani, warejelee madaftari yao ya kumbukumbu na kuikosoa kazi hiyo.

……
……
……..
……..

(P) Andika katika umoja. (alama 2)

Tembe ambazo tulizimeza zilikuwa chungu.

……

(q) Eleza maana za semi au nahau: (alama 2)

(i) kwenda mbweu

……
……

(ii) shika sikio

……
……

(r) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali (alama 4)

Kiatu kilichonunuliwa juzi kimerejeshwa dukani.

4. ISIMU - JAMII

(a) Eleza ukionyesha bayana tofauti baina ya lahaja na lafudhi. (alama 4)

……
……
……
……
……
……

(b) Taja sifa tatu tambulizi za lugha ya misimu (alama 3)

……
……
……

(c) Orodhesha sifa kuu za sajili ya siasa. (alama 3)

……
……
……

Jina: …… Nambari: ……...……

Darasa: ……. Sahihi .....

Tarehe: ……..……

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI

MUDA: 2 ½

MOI HIGH SCHOOL, KABARAK

Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)
KIDATO CHA NNE

MAAGIZO

- Jibu maswali manne pekee. Swali la kwanza ni la lazima
- Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki
- Usijibu maswali **MAWILI** kutoka sehemu moja.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
JUMLA	80	

SWALI LA LAZIMA

77 KWA MAJIBU PIGA SIMU AMA UTUME UJUMBE KWA BWANA CHEPKWONY 0724351706

1.HADITHI FUPI ALAMA 20

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE :Alifa Chokocho Na Dumu Kayanda

Mtihani wa Maisha

1. *"..Acha nijiondokee duniani niwaachie wafanisi wafanikie."*
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. Alama 4
   b) Taja na ufafanue sifa tatu za msemaji. Alama 6
   c) Eleza jinsi maisha ya msemaji yanavyoafiki anwani ya hadithi. Alama 10

2.RIWAYA CHOZI LA HERI : Assumpta Matei ALAMA 20

2. Eleza jinsi **maudhui ya ufisadi** yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya Chozi la Heri. Alama 20
3. *"...liandikwalo ndilo liwalo? Since when has man ever changed his destiny?"*
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. Alama 4
   b) Bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. Alama 6
   c) Kwa kuzingatia hoja **kumi**, jadili jinsi ambavyo hali ya, **" liandikwalo ndilo liwalo"**, inavyojitokeza katika Chozi la Heri. Alama 10.

3.TAMTHILIA KIGOGO : Pauline Kea ALAMA 20

4. "Utawala wa Majoka katika jimbo la Sagamoyo umejaa sumu ya nyoka." Jadili. Alama 20
5. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika tamthilia ya Kigogo
   i) Kinaya Alama 6
   ii) Majazi Alama 8
   iii) Jazanda Alama 6

4.FASIHI SIMULIZI ALAMA 20

6. a) Eleza **aina** tano za wahusika wa fasihi simulizi. Alama 10
   b) Eleza sifa za wahusika wa mighani. Alama 10
7. a) Eleza namna amabavyo hadhira wanahusishwa katika utambaji.Toa hoja nne. Alama 8
   b) Taja na ueleze sifa nne bainifu za hadithi. Alama 4
   c) Taja viungo vinavyopambanua muundo wa nyimbo katika jamii Alama 4
   d) Andika majukumu manne ya nyimbo katika jamii Alama 4

5.USHAIRI ALAMA 20

8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Zitavuma,
Zitakoma,
Nitakwima,
Mti-mle.

Na muda nikisimama,
Nitatongoa nudhuma,
Kwa tenzi zilizo njema,

Nilisifu mti – mle.

Tazipanga tathlitha, tungo zilizo na hekima,
Za huba na thiatha, za kuburudi mitima,
Mashairi mabuthutha, musome mnaosoma.

Mti nishainukia,namea kuwa mzima,
Mizizi yadidimia, ardhini imeuma,
Nanena kitarbia, tungo zilizo adhama
Japo ni tungo za zama, mti-mle hutumia.

Zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,
Dharuba kinitikisa, mti-mle huinama,
Huyumba nikaziasa, matawi yakakingama,
Gharika ikishapisa, hurudi nikawa wima,
Na tungo za takhimisa, mti-mle huzipima.

Maswali

(a) Shairi hili ni la kimapokeo. Toa sababu mbili **kuunga** kauli hii. (Alama.2)
(b) Taja **bahari kuu** ya ushairi ambayo imetumiwa na mshairi. **Fafanua**. (Alama.2)
(c) Fafanua dhamira ya mshairi. (Alama.2)
(d) Kwa kutoa mifano bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (Alama.2)
(e) Eleza jinsi mshairi ametumia idhini ya ushairi katika utungo huu. (Alama.2)
(f) Andika ubeti wa nne kwa lugha natharia. (Alama.4)
(g) Mshairi anamaanisha nini anaposema _zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,‘ (Alama.2)
(h) Eleza toni ya shairi hili. (Alama.2)
(i) Eleza maana ya msamiati ufuatao.
i) Nitatongoa
ii) Zitapusa. (Alama.2)

JINA…… NAMBARI

YAKO…….SHULE……. SAHIHI……

TAREHE……

102/1

KISWAHILI
KARATASI 1
KIDATO CHA NNE
JANUARI
MUDA $1\frac{3}{4}$

SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA PANGANI
KIDATO CHA NNE.
MAAGIZO.

- ***a. Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.***
- ***b. Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.***
- ***c. Kila insha ina alama ishirini.***
- ***d. Kila insha isipungue maneno 400***
- ***e. Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***
- ***f. Insha zote sharti ziandikwe katika kijitabu cha majibu ulichopewa***
- g. ***Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa nakuwa maswali yote yamo***

1. **Lazima**
   Wewe ni miongoni mwa wanahabari wanaomhoji Inspekta Jenerali wa Polisi katika ofisi yake. Andika mahojiano yenu juu ya hatua ambazo zimechukuliwa kuimarisha viwango vya usalama nchini.
2. Jadili umuhimu wa michezo kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Kenya.
3. Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali hii.
   Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa maneno haya: ... ilinichukua muda mrefu mno kuyaamini yaliyonifika.

KISWAHILI
KARATASI 2
KIDATO CHA NNE
JANUARI

SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA PANGANI
KIDATO CHA NNE.
LUGHA
Muda: Saa 2 ½

Jina.....**Nambari ya mtahiniwa**.....

Sahihi ya mtahiniwa.....**Tarehe**.....**Kidato**.....

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali **yote.**
d) Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
g) Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.
h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

1. UFAHAMU:(Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Meli alipokivuka kizingiti cha lango la shule ya kitaifa ya Tungambele alikuwa na azma ya kusoma kwa bidii ili kuinukia kuwa kijana wa kutegemewa na jamii yake. Alikuwa kalelewa katika familia yenye pato wastani. Akasoma kwa juhudi za wazazi wake hadi darasa la nane alipokwangura alama za kumwezesha kujiunga na shule hii ya kifahari. Meli alijua kwamba alikuwa mwanagenzi, si katika masomo ya shule ya upili tu, bali pia katika maisha ya jijini ambamo shule hii ilipatikana. Kwa kweli hii ndiyo ilikuwa mara yake ya kwanza kutia guu kwenye jiji hili ambalo habari zake akizisoma, ama katika magazeti machache yaliyowahi kufika kijijini, au kupitia somo la Elimujamii. Hata hivyo, Meli hakuwa mtu wa kuogopa au kunywea machoni mwa changamoto. Alijiambia kwamba kwa vyovyote vile atapambana na maisha haya mapya.

Saa mbili kamili asubuhi ilimpata Meli kapiga foleni katika afisi ya kuwasajili wanafunzi wageni. Wasiwasi wa aina fulani ulianza kumnyemelea alipotazama hapa na pale bila kuona dalili

ya mja yeyote aliyemfahamu. Alijihisi kama yule kuku mgeni ambaye mwalimu wake alishinda kuwaambia kuwa hakosi kamba mguuni. Hata hivyo aliupiga moyo wake konde na kujiambia kuwa kuja kwake hapa kulitokana na juhudi zake mwenyewe na katu hatauruhusu ugeni wa mazingira kuifisha ari yake ya masomo.

Usajili ulikamilika, naye Meli na wenzake wakajitosa katika ushindani wa kimasomo jinsi waogeleaji wajitumbukizapo kidimbwini wakapiga mbizi, baadhi wakiambulia ushindi na wengine wakifedheheka kwa kushindwa. Meli na wenzake walibainikiwa kwamba wote walikuwa mabingwa kutoka majimbo na wilaya zao. Ilimbidi kila mmoja wao kujikakamua zaidi ili kuelea katika bahari hii ya ushindani. Muhula wa kwanza ulishuhudia kishindo cha Meli kubwagwa chini na majabali wenzake. Alijipata miongoni mwa wanafunzi kumi wa mwisho; au kama alivyozoea **kuwatania** wenzake katika shule ya msingi, "wanafunzi kumi bora kuanzia mwisho"! Hili lilimwatua moyo Meli na kumfanya kutahayari. Alifika kwao amejiinamia kama kondoo aliyeumia malishoni. Akawataka wazazi wake wambadilishie shule lakini wakakataa.

Muhula wa pili na wa tatu mambo yalikuwa yaleyale. Meli akahisi kama askarijeshi aliyeshindwa kabisa kutambua mbinu za kuwavizia maadui. Akaona kwamba njia ya pekee ni kujiunga na wenzake kama yeye katika vitendo vya utundu kama vile kuvuruga masomo kwa kupiga kelele darasani, kupiga soga bwenini na hata kuvuta sigara. Mwanzoni alichukia vitendo hivi lakini alimeza mrututu akisema kwamba ndiyo njia ya pekee ya **kujipurukusha** na aibu. Wazazi wa Meli hawakusita kutambua mabadiliko katika hulka ya mwanao. Wakajaribu kumshika sikio nyumbani lakini akawa hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Wakawahusisha wataalamu wa ushauri nasaha ambao waliwaambia kuwa Meli hakuwa na tatizo lolote la kuyadumu masomo. Kile alichokosa ni kujiamini tu.

Wazazi wa Meli waliona kuwa ni muhimu kuwahusisha walimu katika kutatua tatizo la mwanao. Mwanzo wa muhula wa pili uliwapata wazazi hawa afisini mwa naibu wa mwalimu mkuu. Mazungumzo kati ya wazazi, naibu wa mwalimu mkuu na mwalimu wa darasa la Meli yalidhihirisha kwamba walimu walikuwa wamemuasa Meli kuhusu kujiingiza katika makundi yasiyomfaidi lakini rai zao ziliingia katika masikio yaliyotiwa nta. Aliyopenda Zaidi Meli ni shughuli zilizomtoa nje ya shule kama vile tamasha za mziki, ukariri wa mashairi na drama. Mazungumzo yalibainisha kwamba Meli alihitaji ushauri na uelekezaji Zaidi kutoka kwa mtaalamu wa nasaha pale shuleni.

Meli alianza vikao na mtaalamu huyu ambaye pia alimpendekezea Meli ushauri zaidi kutoka kwa washauri marika. Hili lilimchangamsha zaidi Meli kwani aliwaona hawa kama wenzake waliojua changamoto zake. Juhudi za mtaalamu wa nasaha na washauri marika zilifua dafu. Mwisho wa kidato cha pili ulishuhudia mabadiliko makuu katika hulka na utendaji kimasomo wa Meli. Aliukata kabisa uhusiano wake na marafiki waliompotosha na kuanza kuandamana na wanafunzi waliotia juhudi masomoni. Polepole alama zake ziliimarika. Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne yalimweka kwenye safu ya wanafunzi bora zaidi nchini.

a) "Wanafunzi wawapo shuleni hukumbana na changamoto nyingi". Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hoja <u>sita</u> kutoka kwenye taarifa. .(alama 6)

……

……

……

……

……

……

……

……

.....

.....

b) Eleza mchango wa washikadau mbalimbali katika kumsaidia Meli kupata ufanisi masomoni. (alama 4

……

……

……

……

……

……

……

……

……

c) Bainisha mbinu **tatu** za lugha ambazo msimulizi anatumia katika kuwasilisha ujumbe wake katika kifungu. (alama 3)

……

……

……

……

……

……

d) i. Andika kisawe cha '**kijipurukusha'** kwa mujibu wa taarifa (alama 1)

……

ii. Andika maana ya '**kuwatania'** kulingana na taarifa. (alama 1)

……

……

2 UFUPISHO: (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mfumo wa elimu nchini unatilia mkazo mafunzo mengine ambayo, japo yamo nje ya masomo ya kawaida, yanahusiana na kwenda sambamba na masomo hayo ya kawaida. Vyama vya wanafunzi shuleni vinachangia pakubwa kupitisha mafunzo haya ya ziada.

Vyama vya wanafunzi hutofautiana kulingana na majukumu. Mathalani, vipo vyama vya kidini, vya kitaaluma na vya michezo. Pia, kuna vyama vya kijamii kama vile Chama cha kupambana na matumizi mabaya ya dawa na vya kiuchumi kama vile chama cha Wakulima Chipukizi.

Inadhihirika kwamba vyama vya wanafunzi vina manufaa ya kuhusudiwa. Hii ndiyo sababu shuleni, kila mwanafunzi anahimizwa kujiunga na angaa vyama viwili. Vyama vya wanafunzi huwasaidia kukuza vipawa na kuimarisha stadi za kujieleza. Haya hufikiwa kupitia kwa shughuli za vyama kama vile ukariri wa mashairi mijadala, utegaji na uteguaji wa vitendawili, chemsha bongo na ulumbi. Aidha, vyama hivi huhimiza utangamano miongoni mwa wanachama kwani wao hujiona kuwa watu wenye mwelekeo mmoja. Vilevile utangamano wa kitaifa na kimataifa hujengeka.

Mwanafunzi ambaye amejiunga na vyama vya wanafunzi huweza kukabiliana na changamoto za maisha kuliko yule ambaye hajawahi kujiunga na chama chochote. Katika vyama hivi, wanafunzi hufunzana mikakati na maarifa ya kutatua matatizo na mbinu za kuepuka mitego ya ujana. Kupitia kwa ushauri wa marika kwa mfano, mwanafunzi hushauriwa kuhusu masuala kama vile uteuzi wa marafiki, kuratibu muda, kujikubali na kuwakubali wenzake.

Halikadhalika, mwanafunzi hujifunza maadili ya kijamii na kidini. Kupitia kwa vyama vya kidini na vinginevyo, yeye hujifunza kujistahi na kuwa na stahamala ya kidini, kiitikadi na kikabila. Kadhalika, majukumu ambayo mwanafunzi huenda akapewa hupalilia uwajibikaji, uaminifu na kipawa cha uongozi. Hata anapohitimu masomo yake, mwanafunzi huyu huendeleza sifa hizi.

Vijana wana nafasi kubwa katika kukabiliana na maovu ya kijamii kwani wao ndio wengi Zaidi. Kupitia kwa vyama hivi, wanafunzi wanaweza kuwahamasisha wenza dhidi ya tabia hasi kama vile kushiriki mapenzi kiholela, ulanguzi wa dawa za kulevya na kujiingiza katika burudani zisizofaa. Pia, shughuli na miradi ya vyama hivi huwawezesha wanafunzi kutumia nishati zao kwa njia ya kujinufaisha na kuepuka maovu. Kwa mfano, wanaweza kwenda kukwea milima, kufanya matembezi ya kukusanya pesa za kuwafadhili wahitaji, kuendeleza shughuli za kunadhifisha mazingira na kutembelea vituo vya mayatima na wazee.

Kushiriki katika vyama vya michezo hakumwezeshi mwanafunzi kuimarisha afya na kujenga misuli tu, bali pia huweza kuwa msingi wa kupata chanzo cha riziki baadaye. Wapo wachezaji maarufu ambao walitambua na kuviendeleza vipawa vyao kupitia kwa vyama aina hii, na hivi sasa wana uwezo wa kuyaendesha maisha yao na ya familia zao.

Ifahamike kuwa vyama vya wanafunzi vinapaswa kuwa msingi wa mshikamano na maridhiano. Visitumiwe kama vyombo vya kuwagawa wanafunzi kitabaka. Mwanafunzi hana budi kusawazisha muda anaotumia. Atenge muda wa shughuli za vyama na wa kudurusu masomo yake.

.

a) Fupisha ujumbe wa aya tano za kwanza kwa maneno 80 (alama9,1 ya utiririko)

Matayarisho

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

Nakala Safi

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

b) Fafanua masuala ambayo mwandisi anaibua katika aya tatu za mwisho (maneno 60).

(alama 6, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

……
……
……
……
……

……

……

……

……

……

Nakala Safi

……

……

……

……

……

3. MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40)

a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo: (alama2)
   i) nazali ya kaakaa gumu……...
   ii) kikwamizo ghuna cha kaakaa laini……...
   iii) irabu ya mbele, wastani……..
   iv) kiyeyusho cha midomo……

b) Bainisha silabi katika neno: wachangamshwavyo. (alama 1)
……

c) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kubadilisha nomino zilizopigiwa mstari kuwa vitenzi.
Wachezaji wote watafanyiwa <u>ukaguzi</u> ili kupata <u>suluhu</u> ya matatizo hayo.
(alama 2)

……

d) Andika sentensi ifuatavyo katika umoja.
Tukishiriki katika maigizo hayo vizuri tutaweza kujishindia tuzo.
(alama 2)

……

e) Andika neno **moja** lenye viambajengo vifuatavyo: (alama 2)
nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita,yambwa, mzizi, kauli tendesha,kauli tenda

……

f) Tunga sentensi kuonyesha matumizi yafuatayo ya neno: ni (alama 2)
   i) kitenzi ……
   ii) kiwakilishi
   ……

g) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kivumishi. (alama 2)

…….

h) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.
Nyundo hizo zimetupwa mbali na jumba lile. (alama 1)

……

i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama2)
Nomino ya wingi , kivumishi, kitenzi kishirikishi, kivumishi

…….

j) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo.
Matunda yanayozalishwa kwa njia za kiasili yana virutubishi vingi. (alama 1)
Anza kwa: Virutubishi vingi

…….

k) Tumia viwakilishi badala ya nomino zilizopigiwa mstari.
Mzee atatembelea mji (alama 1)

……

l) Akifikisha sentensi ifuatayo:
basi mwanangu akasema cheusi hivyo ndivyo tunavyoweza kufikia gender parity wewe waonaje (alama 3)

……

……...

m) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi cha wakati.
Idi alijishindia tuzo. Idi alishiriki katika uhifadhi wa mazingira. (alama 1)

.....

n) Tumia 'kwa' katika sentensi kuonyesha: (alama 2)
i) nia

.....

ii) pamoja na

.....

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi.

Upepo ulivuma tulipokuwa tukiondoka. (alama 3)

p) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa.

Rono alicheza gitaa akiwa kwa Kiprono. (alama 2)

.....

q) Onyesha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo:

Mumbi alitia embe kapuni likaiva. (alama 1)

.....

r) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea.

Mmomonyoko wa udongo ulipozuiliwa mashamba yalinawiri. (alama 2)

.....

s) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya **baba na papa** (alama 2)

.....

t) Methali: Haraka haraka haina baraka huambiwa mtu aliye na kasi isiyofaa katika kutenda mambo.Mtu anayepuuza shida za wenzake huambiwa aje? (alama 1)

.....

u) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo: (alama 1)
Wale wageni walikipenda sana.

.....

v) Andika kihisishi cha kuitikia wito kwa mtu wa jinsia ya kike (al 1)
……

w) Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba tendo lilifanikiwa kwa sababu ya kufanikiwa kwa tendo lingine. (alama 1)

.....

x) Andika miundo **miwili** ya nomino katika ngeli ya KI-VI. (alama 1)

.....

y) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari. (alama 1)
Zana hizi zimeundwa <u>na mafundi</u> <u>wenye ustadi mkubwa</u>.

.....

4. ISIMU JAMII: (Alama 10)

a) Umepewa jukumu la kutoa ushauri nasaha(elekezi) kwa kijana mwenzako anayefikiria kujitoa uhai kuhusu manufaa ya kutojitoa uhai. Fafanua sifa **tano** za kimtindo utakazotumia ili kufanikisha mazungumzo yako. (alama 5)

.....
.....
.....
.....

b) Eleza mitindo **mitano** ya matumizi ya lugha katika muktadha wa bunge. (alama 5)

JINA ……NAMBARI YAKO……

SHULE .....SAHIHI ……..……

TAREHE: ……
102/3
SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA PANGANI
MKONDO WA TATU NA MSURURU WA SITA
KIDATO CHA NNE JANUARI
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI

KISWAHILI
KARATASI YA 3
LUGHA
Muda : 2 ½

 KWA MAJIBU PIGA SIMU AMA UTUME UJUMBE KWA BWANA CHEPKWONY 0724351706

MAAGIZO

a) Jibu maswali **manne** pekee.

b) Swali la **kwanza** ni la **lazima.**

c) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zil **tamthilia,hadithi fupi, ushairi** na **fasihi simulizi.**

d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.

e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

f) Kila swali lina alama 20.

g) Karatasi hii ina kurasa **4**

h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zin

SEHEMU A. RIWAYA YA CHOZI LA HERI

1. " …na ikitokea kwamba atauliza swali anakuwa mpokezi wa makonde ,vitisho na matusi ?"

i. Eleza mukatadha wa dondoo hili. (Alama 4)
ii. Taja na ueleze umuhimu wa tamathali ya usemi uliyotumika dondooni. (Alama4)
iii. Mabadiliko ni aushi. Jadili kwa kurejelea riwaya nzima ya Chozi la Heri. (alama 12)

SEHEMU B. TAMTHILIA YA KIGOGO. (Alama 20)

2. "Kama mmeletwa hapa na umbeya,naona mmekosa njia"

(a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (Alama 4)

(b) Jadili jinsi ambavyo msemaji na wenzake wenye hulka sawia walivyopotea njia.

(Alama 5)

(c) Eleza dhima sawia za wasemewa. (Alama 5)

(d) Eleza vizingiti vyovyote sita wanavyopitia wanaharakati tamthiliani. (Alama 6)

3. Jadili mbinu zifuatazo kama zilvyotumika katika tamthilia ya kigogo. (alama 20)

a. Uwili
b. Jazanda
c. Majazi
d. Tashtiti

SEHEMU C. TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINEZO

4. " Nafurahi maana najua hakuna mtoto mwengine wa mtu atakayekatishwa tamaa na …"

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
b. Onesha kinaya kinavyojitokeza katika dondoo. (Alama2)
c. Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi ya mwalimu mstaafu. Thibitisha. (alama 14)

5. Vijana wamekumbwa na changamoto nyingi katika jamii. Tathmini kauli hii ukirejelea hadithi zifuatazo.

Tulipokutana tena.

Mtihani wa maisha

Shogake dada ana ndevu

Ndoa ya mashaka

SEHEMU D. FASIHI SIMULIZI (ALAMA 20)

6. Dunia hadaa,ulimwengu shujaa.Mnachohitaji mlipofikia, ni ujasiri wa simba kuyakabili maisha.Adabu na bidii yenu leo, ni miche itakayozaa matunda, matunda matamu ya maisha mema kesho.Sitaki muziandame nyendo potovu . Mtakuwa mnajiponza wenyewe ; na hilo litakuwa sawa na kuutumbukiza mustakabali wenu kwenye shimo lenye kina kirefu na giza totoro.Jueni ujana ni moshi na ukienda haurudi.

(a)

i. Tambua kipera hiki na utoe ithibati. (Alama 2)
ii. Ni sifa zipi za kipera hiki zilizojitokeza hapom juu. Eleza kikamilifu (alama 5)

(b) Misimu hutumia mbinu anuwai katika uundaji wake. Taja tano na utolee mifano mwafaka.. (Alama 5)

(c) Eleza mbinu ambazo ungetumia kufanikisha kipera hiki. (Alama 8)

7.

a) Eleza maana ya miviga. (Alama 2)
b) Taja sifa tano za miviga. (Alama 5)
c) Pendekeza njia tatu za kuhifadhi kipera cha miviga. (alam 3)
d) Eleza udhaifu wa mbinu zifuatazoza ukusanyaji data ya fasihi simulizi.
   (i) Hojaji (alama3)
   (ii) Kushiriki (alama 3)

e) Fafanua matatizo yanayomkabili mtafiti wa fasihi simulizi nyanjani. (alama 4)

SEHEMU E. USHAIRI

Swali 8.

Hakika siku ya leo, ni siku ya majivuno
Basi pasiwe na choyo, na usonono
Tulekezane yaliyo, unawiri Muungano.

Tuzisafisheni nyoyo, pasiwe na miguguno
Yaongoke tutakayo, kusiwe na mabishano
Mbegu hii tupandayo, ilete mema mavuno.

Tufungulie upeo, Mola usiye mfano
Pa kitasa na komeo, tupite bila kinzano
Tupitishe njia hiyo, pasina masongamano

Twakuomba uumbao, mkono vyanda vitano
Tushikane hii leo, tuwe moja tangamano
Tupendane kwa pumbao, hali na maridhiano

Aliye ana machukiyo, adui wa Muungano
Naazibe masikiyo, asisikie maneno
Kisha awe kibogoyo, asiwe na moja jino.

Ya Ilahi ujalie, juu wetu Muungano
Nuru yake izagae, na nguvu za mapigano
Hasidi mpe hakie, mateso yaso mfano

Watamati komeleo, kuimba kwangu hukuno
Nataka maendeleo, yasiyo na malumbano
Daima tuwe ni ngao, palipo msagurano

(i) Huku ukitoa mifano thibitisha kuwa shairi hili ni sala. (alama 4
(ii) Liweke shairi hili katika bahari mbili ukitumia: (alama 2)
Idadi ya

(i) Mishororo
(ii) Vina
(iii) Onyesha muundo wa shairi hili. (alama 5)

(iv) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 3)

(v)ukitoa mifano eleza umuhimu wa idhini zifuatazo kama zilivyotunika katika shairi. (Alama 4)

a) Inkisari
b) Mazda
c) Kuboronga sarufi
d) Tabdila

(vi) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)

(i) Usonono –
(ii) Msagurano –

SHULE YA UPILI YA SUNSHINE

KISWAHILI
KIDATO CHA 4
KARATASI 2
MUDA: SAA 2 ½

JINA ……. NAMBARI YA MTAHINIWA……..

DAHASA:……

Maagizo:

a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Jibu maswali yote .
c) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
d) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha za Kiswahili .
e) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.

Kwa matumizi ya mtahini **pekee**

SWALI	UPEO	ALAMA

UFAHAMU		
UFUPISHO		
SARUFI		
ISIMU JAMII		
JUMLA		

UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Ilikuwa jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa Taarifa ya habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe pesa za kiinua mgongo. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi lake mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki. Watu wengi walinishawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, Waziri wa Kilimo alitangaza bei mpya. Shilingi 1,500 kwa kila gunia. name nilikuwa naanza kuumakimikia mradi huu.

Baada ya tarifa, nilikoga, nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichulua mara moha. Usingizi niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kilimo nilitenga ekari kumu za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikati ya mwezi wa Machi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa manyakanga wa kilimo, nilipa shilling elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejeo. Kwanza, nililipa shilling 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunu amagunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilling 3,300 kila gunia. Mwzi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda. Ili nipate mazao bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilling 1,000 kila ekari. Mvua ilinesha vizuri na baada ya siku saba mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mebgu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua wa kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilal kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yananifikia magotini. Hii ikawa ishara kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo ‘amonia’. Gharama yake ikawa shilling 1,300 kila gunia. Hivyo, nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano.

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa maisha. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapita njia waliajabia mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siwanawaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanzi wanfu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno nitakayopata kukadiria faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa ‘Usikate majani, mnyama hajauawa.’

Bila taarifa wala tahadhari mvua ikatoweka. Hayakupita majuma mawili mahinda yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahind, shamba ilkageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makasio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi yfanyavyo moshi.

Lakini ‘Muumba ndiye Muumbua’. Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha.Muda si muda mahind yalianaza kunawiri. Kumbe tukio lililonivunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwaa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafu huku majani ya mahindi yamechanika kama nyuzi. Niliugua. Baada ya wiki moja, nilipata nafuu. Nilipotazama upande wa shamba nikaona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli. Muda sio mferu mahindi yalirudi hali yake tena, kisha yakakomaa. Haraka za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli kii ikawa shilingi 5,000. Kuvuna, kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500. Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. habari motomoto siku hiyo ilikuwa: “MAHIND GUNIA 900/-” Niligutuka usingizini.

Maswali

(a) Andika kichwa mwafaka kwa kifungu hiki cha habari. (al 1)

……..

(b) Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika? (al 1)

……..

(c) Taja matatizo matatu yaliyotisha mradi wa msimulizi wa kukuza mahindi. (al 3)

……..

……..

……..

……..

(d) Eleza maana ya methali zifuatazo:

(i) Usikate majani, mnyama hajauawa

……..

……..

……..

(ii) Muumba ndiye muumbua

……..

……..

……..

(e) Eleza mambo mawili yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia. (al 2)

……..

……..

……..

……..

(f) Kwa nini msimulizi alisem maumbile ni kitu cha ajabu? (al 2)

……..

……..

……..

(g) Eleza maana ya:

(i) kiinua mgongo

……..

(ii) manyakanga wa kilimo

……..

UFUPISHO

Soma makala yafuiatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Wakati mmoja, nchi za bara la Afrika zilitawaliwa na mchi za kimafharibi – Uingereza, Ujerumanii, Ufaranza n.k. Japo sasa nchi hizi zimejinyakulia uhur, serikali zao zinashabihianan na serikali za watawala wao wa hapo awali.

Wamishonari, wakoloni na walowezi walipokuja Afrika, waliwakuta watawala wa Kiafrika. Sehemu kama Uganda na Uhebeshi zilikuwa na tawala za kifalme. Ijapokuwa Kenya haikuwa na mfalme, kila kundi la watu au kijiji kilichagua kiongozi wao, ambaye mara nyingi alikuwa ni mtu aliyeheshimiwa kwa ushujaa wake au kwa busara yake. Kiongozi, japo hakuchaguliwa kw akura za watu wote kijijini, aliteuliwa na baraza la wazee wa kijiji kwa niaba ya wakazi wa kijiji. Kwa mfano Bunganda, Kabak alikuwa akiba wa bara na baraza la machifu baada ya kufa Kabaka aliyetangualia, ijapokuwa mwenyewe alikuwa ni mrithi wa kiti.

Katika nchi ambazo hazikutawaliwa na wakoloni, kama vile Uhabeshi, tungetumaini kuona mtindo wao wa asili wa kiutawala ukidumu lakini pia wao walilazimik akuugeuza kidogo ili ukidhi mahitaji na maendeleo ya kisasa ulimwenguni. Hata hivyo, serikali ya Uhabeshi ilidumu sana kwa muda mrefu na ni majowapo ya serikali zilizokuwa thabiti kabisa barani Afrika.

Wakoloni walipotawala waliwanyima wazee na machifu uwezo wa kuchagua viongozi waliowapenda. Kusema kweli, waliyavunja mabaraza ya wazee. Chifu sasa angeteuliwa na Mkuu wa wilaya.

Ili waweze kutawala kwa urahisi, wakoloni walitumia siasa ua "tenda tawala' ambayo wananchi waligawanywa katika makundi ya kikabila, jambo ambalo athari zake mbaya zinaendelezwa hadi leo.

Baada ya kujinyakulia uhuru, Waafrika walianza kujitawala. Serikali walizounda zilifumbata utaratibu ulu ule wa watawala wao waliondoka. Kwa mfano, kama ni Mwindereza, serikali hiyo mpya ilifuata utaratibu wa Kiingereza katika sheria na mambo mengineyo.

(i) Eleza ujumbe wa mwandishi katika aya za kwanza tatu (maneno 70) (alama 9, 1 mtiririko)

Nakala chafu

……..
……..
……..
……..
……..
……..
……..
……..
……..
……..
……..

Nakala safi

……..
……..
……..
……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

(ii) Kwa kujerelea aya za mwisho tatu eleza mbinu ambazo wakoloni walitumia kurahihisha utawala wao katika mchi za Afrika. (maneno 40) (Alama 6, 1 ya mtitiriko)

Nakala chafu

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

Nakala safi

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

SARUFI (ALAMA 40)

(a) Taja na kutofautisha irabu za mbele. (al 2)

……..

……..

(b) Tung asentensi MOJA kubainisha maana mbili za neno kikosi. (al 2)

……..

……..

(c) Andika katika wingi: (al 1)

Jino langu bovu linaloniuma linanitatiza.

……..

……..

(d) Tumia kielezi cha wakati badala ya kielezi kilichotumika katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Watalii walitutembelea mjini Nakuru

……..

……..

(e) Geuza sentenzi zifuatazo ziwe katika hali zilizoonyeshwa mabanoni. (al 2)

(i) Maimuna anapika wali (wakati uliopo hali isiyodhihirika).

……..

(ii) Wao walisoma riwaya hiyo (watatu ujao hali ……)

……..

(f) Tumia nomino zifuatazo za kawaida kuunda nomino za jamii. (al 2)

I. Viwavi

……..

II. Zabibu

……..

(g) Tunga sentensi kuonyesga matumizi ya fuatayo ya neno KAMA. (al 2)

I. Kihusishi

……..

II. Kitenzi

……..

(h) Unda neno lenye muundo ufuatao. (al 2)

nafsi ya kwanza umoja, hali timilifu, mtendewa, mzizi, kauli tendea, kauli tenda

……..

……..

(i) Tunga sentenzi yenye mundo ufuatao. (al 2)
KN (V+ n + V) + KI (t + V)

……..

……..

(j) Bainisha maana mbili za sentesi ifuatayo: (al 2)
Viti vingine vimeletwa

……..

……..

(k) Changanua sentenzi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali. (al 4)

Jirani mwema amenipa maziwa

……..

……..

……..

……..

……..

(l) Onyesha silabi ya kuwekewa shadda katika neno msingi. (al 1)

……..

(m) Bainsiha aina za virai vilivyopigwa mstari (al 2)

Mwanafunzi mtukutu atashauriwa na Bw. Ali.

……..

……..

(n) Tunga sentensi inayedhihirisha: (al 2)

I. dhamira arifu

II. dhamira tegemezi

……..

……..

(o) Andika katika udogo umoja (al 2)

Nyundo zilizokuwa pamoja madebe haya zimeibwa na wezi wale

……..

……..

(p) Tambua vivunganishi na utaje aina yake (al 2)

I. Swali hilo limemshinda mwalimu seuze wewe

……..

II. Kaka ameniita kwa kunituma

……..

(q) Ainisha vitenzi katika sentenzi ifuatayo. (al 2)

Fanani aamekura akiwatumbuiza wageni jukwaani

……..

……..

(r) Kanusha sentensi:

Bawabu huyu amekuwa akitaka kuacha kazi tangu mwaka jana.

……..

……..

(s) Onyesha shamirisho katika sentensi ifuatayo. (al 3)

Adika alibebewa viazi na Amina kwa torohi.

……..

(t) Andika kinyume cha sentensi: (al 2)

Hamisi alimwoa Khadija akiwa amelewa

……..

……..

1. Jadili mitazamo au nadharia tano zinazofafanua chombuko au asili ya Kiswahili. (al 5)

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

2. Eleza umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya taifa. (al 5)

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

SHULE YA UPILI YA SUNSHINE

102/3
KISWAHILI
FASIHI YA KISWAHILI
JANUARI
MUDA: 2 ½

JINA: ……...NAMBA YAKO:……

DARASA ……SAHIHI YA MTAHINIWA …….

Maagizo

 KWA MAJIBU PIGA SIMU AMA UTUME UJUMBE KWA BWANA CHEPKWONY 0724351706

1. Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

2. Jibu maswali manne pekee.

3. Swali la kwanza ni la lazima.

4. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki: Ushairi, Riwaya, Hadithi Fupi na Fasihi simulizi.

5. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

TAMTHILIA

1. Kigogo

Tamthilia ya Kigogo ni ‘kioo’ cha hali halisi ya mambo barani Afrika. Jadili. (al 20)

SHAIRI

2. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Nilicheza ujanani, nisikieni wendani
Nimeishi duniani, zaidi nyaka sitini
Sikufanya cha manani, kiniponye uzeeni
Nilicheza ujanani, ninalipa uzeeni

Nilicheza ujanani, haiza kwenda shuleni
Waloenda darasani, sasa wako magarini
Wananipita njiani, wakinipiga honi
Nilicheza ujanani, ninalipa uzeeni

Nilicheza ujanani, haiza kwenda shambani
Hakataa kutuwani, jembe liwe mikononi
Na sasa niko njaani, wenzangu wako shibeni
Nilicheza ujanani, ninalipa uzeeni

Nilicheza ujanani, haiza kwenda sokoni
Waliouza juani, sasa wala vivulini
Na mimi sina thumuni, initoe mashakani
Nilicheza ujanani, ninalipa uzeeni

Nilicheza ujanani, ndoa sikuthamini
Waliooa yakini, niliwaona watini
Sasa niko ukongweni, bila yeyote nyumbani
Nilicheza ujanani, ninalipa uzeeni

Nilicheza ujanani, kutwa kucha magomani
Niliharibu mapeni, ulevini danguroni
Niliufanya uhuni, bila kuola usoni
Nilichjeza ujanani, ninalipa uzeeni

Nilicheza ujanani, sasa niko kilioni
Ninalala kibandani, sina mali asilani
Sina watoto olani, wala chakula ghalani
Nilicheza ujanani, ninalipa uzeeni

Nilicheza ujanani, sasa najuta Fulani
Machozi tele machoni, sina wa kuniauni
Ninamuomba Manani, anionee Imani
Ninacheza ujanani, ninalipa uzeeni

Maswali

(a) Eleza toni ya shairi hili. (al 2)

(b) Fafanua umbo la shairi hili. (al 4)

(c) Fafanua mambo matano ambayo msharii aliyapuuza akiwa kijana na namna anavyoathiriwa nayo. (al 5)

(d) Fafanua bahari katika shairi hili. (al 3)

(e) Andika ubeti wa sita katika lugha ya nathari. (al 4)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili. (al 2)
(i) Danguroni
(ii) kuola

AU

3. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Mwili na fahamu
zilikuwa kitandani
Usingizini mnono

Ghafla, ikaha ndoto
Ndoto ya kutisha
Na kubabaisha
Ndoto ya jasho
Na joto kali-
Jinamizi!

Kaumu ya watu
Ikibeba shoka
Panga kali
Na misumeno inayonguruma
Ilikuja kwa mawimbi
Na bila huruma
Ikajinja miti
Na kunyunga chemichemi
Ikiimba wimbo
Za mashamba na mbao

Ardhi iliachwa uchi
Kama mkazi wa kijiji
Aliyeshambuliwa njiani
Na kundi la majambazi

Kijinga cha jua
Kiliunguza udongo,
Viganja vya upepo
Viliufikicha kwa nguvu
vumbi jekundu
Lilanza kupaa angani
Kama wimbo wa matanga
Katika kijiji ambacho
Kinatawaliwa na kipindipindu

Mvua ilikuja kwa hasira
Kwa kucha zake ndefu
Ilihujumu ardhi
Na kuacha majeraha
Yatiririka damu
Polepole, ardhi nzima
Ilegeuka bahari
Siyo ya maji ya chumvi
Siyo ya mikamba na sulisuli
Bali mawimbi makuu
Ya machanga na vumbi

Povu lilirushwa
Na kutua juu ya mawe
Tanzu za miti
Na nywele
Mvua ilipokuja tena
Katika mashamba
Pojo na mbaazi
Zilikwama njiani
Ya maisha

Katika kijiji
Ng'ombe, kondoo na mbuzi
Walibadilika sura
Na kuwa mafupa
Yanayojisukuma njiani
Kama makobe makongwe

Kama abiria
Katika dau
Katika bahari ya kusi
Binadamu, wanyama
Mimea, wadudu na ndege
Walitingishwatingishwa
Na kusukwasukwa
Na bahari ya mashaka

Wingu la huzuni
Lilifunika vijiji
Kama wingu la anga
Likifunika vilima

Mazizini na njiani
Waliangkiana magombe
Kama majani makavu
Yakiangushwa na upepo
Majira ya mpukutiko

Katika nyua za kijiji
Machozzi yalibubujika
Kama maji maasi
Kutoka mifereji iliyopasuka

Walizikwa watoto
Na wazee
Na hatimaye samba
Ambao kabla ya janga
Walingara kwa afya

Kupitia ukungu mwekundu
Sauti ya kejeli
Ilisikika, ikiimba
Ndimi jangwa
Niogopewa na mvua
Ndimi jangwa
Ninyongaye mito
Ndimi jangwa
Ninyimaye mayai, maziwa na nyama
Ndimi jangwa
Nihiniye mboga, nafaka na matunda
Ndimi jangwa
Mtawala weni!

Maswali

(a) Hili ni shairi gani? Dhihirisha. (al 2)

(b) Huku ukitoa mifano kwenye shairi hili, eleza sifa mbili za mashairi ya aina hii. (al 2)

(c) Mshairi anazungumzia nini katika shairi hili? (al 1)

(d) Fafanua athari ya anachokizungumzia mshairi katika shairi hili. (al 6)

(e) Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza taswira mbalimbali katika shairi. (al 4)

(f) Huku ukitoa mifano kwenye shairi, onyesha matumizi ya mishata katika shairi. (al 2)

(g) Huku ukitoa mifano mwafaka, taja tamathali mbili zilizotumiwa katika shairi. (al 2)

(h) Eleza maana ya kauli ifuatayo; Mazizini na njiani yaliangukianan magombe. (al 1)

RIWAYA

Chozi la Heri

4. Anwani “Chozi la Heri” inaafiki riwaya hii. Thibitisha. (al 20)

AU

5. “Ni kweli, mama ana haki ya kusamehewa kwani hakuna binadamu hata mmoja aliyekamilika.”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)

(b) Jadili umuhimu wa mzungumzaji katika riwaya hii. (al 6)

(c) Fafanua maudhui ya ukatili kama yalivyosawiriwa katika riwya ya Chozi la Heri. (al 10)

HADITHI FUPI

Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine

6. Ndoto ya Mashaka (Ali Abdulla Ali)

Jadili mashaka ya Mashaka katika hadithi ya 'ndoto ya Mashaka'. (al 20)

AU

7. Mtihani wa Maisha (Eunice Kimaliro)

"Nimeuza ng'ombe wangapi kwa ajili ya kisomo chako kumbe wewe ni mbumbumbu huna kumbukumbu?"

(a) Andika muktadha wa dondoo hili. (al 4)

(b) Kwa kurejelea hadithi hii, onyesha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari. (al 4)

(c) Bainisha matumizi ya kinaya katika hadithi hii. (al 12)

8. FASIHI SIMULIZI (al 20)

(a) Eleza maana ya 'malumbano ya utani'. (al 1)

(b) Jadili sifa tano za malumbano ya utani. (al 5)

(c) Bembelezi ni nyimbo za kuwabembeleza watoto ili walale au kunyamaza wanapolia. Fafanua aina nyingine kumi za nyimbo. (al 10)

(d) Nyimbo zina hasara gani katika jamii? (al 4)

KWA MAJIBU PIGA SIMU AMA UTUME UJUMBE KWA BWANA CHEPKWONY 0724351706